KUFANYWA WANA WENYE MAMLAKA *1*

. . . nijisikie vizuri kusikia hivyo, hilo ni jema. Vema, ni kila wakati, kama nilivyosema hapo awali, “Nilifurahi waliponiambia, ‘Twendeni katika nyumba ya Bwana.’” Ninaamini Daudi ndiye aliyetoa tamshi hilo wakati mmoja, “Na twende nyumbani kwa Bwana.” Sijui mahali popote pazuri zaidi kuwepo, nawe je, kuliko katika nyumba ya Bwana.

2 Sasa, usiku wa leo, tuna marafiki hapa ambao wametoka mbali sana huko Georgia. Labda wataondoka kwa magari baada—baada ya chakula cha mchana usiku wa leo. Na halafu tutaninii . . . Wengine wao wanatoka mbali sana, natumai mtabaki. Basi mumekaribishwa katika vyumba tulivyo navyo.

3 Halafu Jumatano usiku tutaendelea na hili, hili somo, halafu, Bwana akipenda, Jumapili ijayo tena.

4 Na halafu Chautauqua utaanza tarehe sita. Kwa hiyo nyote ambao mumeishapanga likizo yenu, tunatarajia wakati mzuri sana, huko Chautauqua. Huko ndiko sisi kwa kawaida huwa na wakati mzuri sana. Si makundi makubwa sana, wakati mwingine sisi hufikia . . . Itachukua kufikia yapata . . . Nadhani tungeweza kuingiza watu elfu kumi mle ndani, kwa urahisi. Lakini, kwa kawaida, mwaka uliopita nafikiri tulikuwa na yapata watu elfu saba, kitu kama hicho. Palikuwa pamejaa watu, lakini kuna nafasi kubwa ya kusimama. Na viti ambavyo wangeweza kuviweka kila mahali kandokando. Na kwa hivyo tunautazamia huo.

5 Nasi tuna furaha kuona wengi wa ndugu zetu wahubiri humu. Siwezi kamwe kukumbuka jina lake hapa, yule mmishenari, Ndugu Humes na Dada Humes, huyo ni wewe unayeketi papa hapa, na watoto, tunafurahi kuwa pamoja nao, mmishenari. Wengine, Ndugu Pat, Ndugu Daulton, na, loo, wengi sana tu, Ndugu Beeler. Na nimemwona Ndugu Collins muda mfupi tu uliopita. Na, loo, kwa namna fulani ingekuwa vigumu kuwataja wote. Lakini tuna furaha sana kuwa nanyi katika nyumba ya Bwana usiku wa leo. Huyu Ndugu Neville ambaye ni mtu wa thamani aketiye nyuma yangu hapa ili kuomba pamoja nami huku tunapoenda kufundisha Neno. Charlie, nafurahi kukuona na Dada Nellie hapa usiku wa leo, hao watoto wadogo. Hii ni . . . na kufundisha Biblia kwa kawaida ni ninii sana . . . Naam, Ndugu Welch, mimi tu . . . nilikuwa ninakutafuta, nakuona umeketi huko nyuma sasa.

6 Kufundisha Biblia kwa kawaida ni hatari kidogo, kidogo, mwajua, ni kama kutembea juu ya barafu nyembamba, kama tusemavyo. Lakini tunajisikia tu ya kwamba labda, hapa tulipofikia na wakati huu, ingefaa kwa namna fulani kulileta ka—kanisa kwenye kile ninachowazia, kufikia ufahamu m—mkamilifu, mahali petu, kuhusu kile tulicho katika Kristo Yesu. Na wakati mwingine nafikiri kwamba kuhubiri ni jambo zuri sana, bali naamini wakati mwingine, Ndugu Beeler, kwamba kufundisha kunapita jambo hilo, kwa namna fulani. . .hasa kwa kanisa.

Sasa, kwa kawaida kuhubiri humnasa mwenye dhambi, kunamleta chini ya hukumu kwa Neno. Bali kufundisha humweka mtu mahali pake kile alicho. Nasi kamwe hatuwezi kuwa na imani sawasawa mpaka tujue mahali petu kwamba sisi ni akina nani.

7 Sasa, kama Marekani, nchi hii nzuri hapa, ilinituma Urusi, kama balozi wa taifa hili, huko Urusi, basi kama wao wamenituma Urusi kirasmi, uwezo wote ilio nao Marekani uko nyuma yangu. Neno langu ni kama tu la Marekani, kama nimetambuliwa kama balozi.

8 Ndipo basi kama Mungu ametutuma kuwa mabalozi Wake, uwezo wote ulio Mbinguni, yote aliyo Mungu, Malaika Wake wote na uwezo Wake wote unasimama nyuma ya maneno yetu kama sisi ni wajumbe waliotawazwa vizuri, na kutumwa kwa watu. Inambidi Mungu kuheshimu Neno, kwa kuwa Yeye ameandika kwa uchaji sana, kwamba "Lolote mlifungalo duniani, hilo nitalifunga Mbinguni. Lolote mtakalofungua duniani, hilo nitalifungua Mbinguni. Nami ninawapa ninyi funguo za Ufalme." Loo, ahadi kubwa jinsi gani Yeye alilolipa kanisa!

9 Nami, baada ya hivi majuzi. . .Wengi wenu, nadhani, walikuwa hapa asubuhi ya leo kusikiliza kama nilivyojaribu, kwa njia yangu nyenyekevu, rahisi, kuelezea li—lile ono nililoona la Mbinguni.

10 Bila shaka nisingejaribu kamwe kutilia shaka jambo lolote mtu yeyote alilowahi kuniambia kwamba Mungu aliwaambia. Ningeamini jambo hilo hata ingawa sikuliona katika Maandiko, bado ningalitaka kuamini neno la ndugu huyo. Hu—huenda ningedumu tu na Biblia, bali hata hivyo ningeamini kwamba labda ndugu alilielewa vibaya kwa njia fulani, kwamba huenda ikawa alitatizika kidogo. Na hata hivyo ningeliamini yeye—yeye kuwa ni ndugu yangu.

11 Na kama kuna jambo linalochoma moyoni mwangu, nami natumainia halitaondoka katika miaka yangu ijayo, kwamba sitasahau kamwe jambo lililotukia asubuhi ya Jumapili iliyopita, yapata juma moja. Limenifanyia jambo fulani ambalo limebadilisha maisha yangu kabisa. Si—siogopi. Si—sina hofu

hata kidogo ya kufa. Kifo hakitishi hata kidogo. Na ha—hakitishi kwako kama tu ungelifahamu. Sasa, labda kama. . .Itakubidi kupata tukio hilo upate kujua jambo hilo, kwa sababu hakuna njia ya kulielezea. Huwezi kupata maneno, kwa sababu hayamo katika kamusi ya Kiingereza, wala kamusi nyingine yoyote, kwa sababu ni jambo lililo katika Umilele; hakuna jana, hakuna kesho, yote ni wakati uliopo. Na si eti “Najisikia vizuri sana,” na saa moja tangu sasa, “Sijisikii vizuri sana,” na saa nyingine, “najisikia vizuri tena.” Ni wakati uliopo wakati wote. Unaona? Hakuna kikomo, ni amani hiyo tukufu tu, kitu fulani.

12 Na hapawezi kuwepo na dhambi, hapawezi kuwepo na wivu, hapawezi kuwepo na ugonjwa, hakuna—hakuna chochote kingeliweza kufika katika hiyo pwani ya Mbinguni. Na kama naweza kuwa na majaliwa ya kusema hili, ambapo, labda sina. Kama sina, basi naomba Mungu anisamehe. Bali kama nina hayo majaliwa, na iwe kwamba Mungu aliniruhusu kutwaliwa nipate kuona jambo fulani, ningerejea kwenye Mbingu za kwanza. Na basi ninaamini, mtu mmoja katika Biblia, jina lake, naamini lilikuwa ni Paulo, ambaye alitwaliwa hata Mbingu za tatu. Na kama ilikuwa yenye utukufu jinsi hii katika Mbingu ya kwanza, hiyo Mbingu ya tatu ina mambo gani? Si ajabu hangeweza kunena habari zake kwa miaka kumi na minne! Alisema hakujua kama alikuwa katika mwili au nje ya mwili. Pamoja na huyo mtume mkuu, si kushiriki cheo cha—cha—chake, wala si kujaribu hata kidogo kujifanya wenyewe jinsi alivyokuwa, bali naweza kusema pamoja naye, sijui kama ilikuwa katika mwili huu au nje ya mwili. Jambo tu ni kwamba, ilikuwa halisi tu kama ninavyowaangalia.

13 Na daima nimeshangaa kuhusu kama ningepitia karibu na kuona wingu dogo likielea karibu, roho fulani, na kusema, “Hao hapo ndugu na dada wanaenda zao, huyo ni Charlie na Nellie. Hao hapo Ndugu na Dada Spencer wanaenda kule.” Hilo daima limeniduwaza. Kama macho yangu yamo kaburini, yakioza, yakivunda, kama masikio yangu hayako hapa kusikia tena, na kama damu yangu yote imerudi nao wameuhifadhi kwa dawa, nao uko majini ama ardhini, na akili zangu, chembechembe zote za ubongo wangu zimeangamia, basi nawezaje kuwa chochote ila roho anayeelea huku na huko? Na jambo hilo lilinisumbua mno. Jinsi nitakavyopenda kusema, “Alo, Ndugu Pat, loo, nina furaha sana kukuona! Alo, Ndugu Neville, jinsi ningependa kukuona!” Lakini nikawaza, “Vema, iwapo sitakuwa na kitu cha kuonea, kinywa chochote cha kunenea, kimeoza, ni vumbi, ningewezaje kusema, ‘Habari yako, Ndugu Pat,’ ‘Habari yako, Ndugu Neville,’ ama kadhalika, ‘Habari, Charlie’?”

14 Lakini sasa ninajua ya kwamba hilo ni kosa. Kwa kuwa imeandikwa katika Maandiko, ambayo nasema hayalipingi, “Kwa kuwa nyumba ya maskani yetu ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja tayari inayongoja,” nyumba nyingine ya maskani

iliyo na macho, maskio, midomo, akili. “Kama nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa!” Ina mwili ninaoweza kugusa, unaoweza kuongea.

15 Na sasa nimekumbuka, sasa hivi, ya kwamba Musa alikuwa amekufa na katika kaburi lisilojulikana kwa miaka mia nane, na Elisha alikuwa ameenda Mbinguni miaka mia tano hapo awali, lakini kwenye ule Mlima wa Kugeuzwa walionekana wakizungumza na Yesu.

16 Baada ya Samueli kufa kwa yapata miaka mitatu hadi mitano, na yule mchawi wa Endori akamwita, naye akaanguka kifudifudi, kisha akasema, “Umenidanganya, kwa kuwa wewe ni Sauli, wewe mwenyewe.” Akasema, “Kwa kuwa naona miungu!” Yeye alikuwa kafiri, unaona. “Ninaona miungu ikiinuka.”

17 Naye Sauli hakuweza kumwona bado, ndipo akasema, “Anafananaje? Nielezee alivyo.”

Kasema, “Amekonda, naye ana vazi begani mwake.”

18 Kasema, “Huyo ni Samueli, nabii, mlete hapa mbele zangu.” Nami nataka muone kwamba Samueli hakuwa amepoteza hulka yake yoyote. Alikuwa angali ni nabii. Alimwambia Sauli yale hasa yangetukia siku iliyofuata.

19 Kwa hiyo, mnaona, kifo hakitutokomezi kabisa tunapolia na kuomboleza na kuhuzunika kaburini. Hubadilisha tu makao yetu. Kinatutoa kutoka mahali fulani hata . . . Umri ni kitu gani? Kama nikiishi saa moja zaidi, nitaishi zaidi ya watu wengi wenye umri wa miaka kumi na sita, nitaishi zaidi ya watu wengi wenye umri wa miaka mitano. Umri si kitu. Tumewekwa tu hapa kwa kusudi fulani, kutekeleza jambo fulani.

20 Vema, sasa, wengi wa hawa akina mama wenye nyuso nzuri walioketi hapa, baadhi yao wenye umri wa miaka sitini au sabini, wangesema, “Vema, nimefanya nini, Ndugu Branham?” Umewalea watoto wako. Umefanya ulilopaswa kufanya.

21 Labda baba fulani mzee anayeketi hapa, aseme, “Vema, nimelima mashamba, nimefanya *hivi*. Sikuhubiri kamwe.” Lakini wewe ulifanya yale tu ambayo Mungu alikutuma ukafanye. Kuna mahali kwa ajili yako.

22 Nikizungumza na daktari mzee, jana, mmoja wa madaktari rafiki zangu, rafiki wasiri, mwenye umri wa miaka themanini na kitu. Na shemeji yake wa kike yuko hapa kanisani usiku wa leo, naye amekuwa na wasiwasi kidogo, kidogo tu juu yake. Nami nilienda kumwona. Na mara nilipoanza kuzungumza naye, akachangamka, akaniambia habari za safari ya kuwinda aliyofanya miaka mingi iliyopita huko Colorado, nchi ile ile ninayowindia mimi. Akiwa tu mchangamfu na mwenye furaha! Nami nikasema, “Daktari, umefanya kazi miaka mingapi?”

23 Akasema, “Ulipokuwa unanyonya.” Na kule chini kabisa nikasema . . . “Na mara nyingi,” akasema, “nimefanya kazi,

nachukua gari langu la farasi, naweka matandiko juu ya farasi wangu. Nikachukua mfuko mdogo na nimetembea."

24 Nami nikasema, "Ndiyo, kuelekea ukingoni mwa vijito, saa nane usiku, ukiwa na tochi yako, ukijaribu kuipata nyumba ambamo mtoto mdogo anaumwa na tumbo au mama aliye na utungu wa kuzaa."

"Hiyo ni kweli."

25 Nami nikasema, "Wajua, daktari, ninaamini, nga'mbo ya mstari huu hapa unaogawanya, kati ya kupatikana na mauti na kutokupatikana na mauti, Mungu ana mahali kwa ajili ya madaktari wazee waliotumika namna hiyo."

26 Machozi makubwa yakamjia machoni mwake naye akaanza kulia, akainua mikono yake minyonge akasema, "Ndugu, natumaini ndivyo ilivyo." Ng'ambo ya pili, Mungu huihukumu nafsi ya mwanadamu, jinsi alivyo.

27 Ndipo nikampa Andiko hili linaloridhisha. Mara nyingi, ukijaribu kulima katika mashamba hayo yenye giza na matope usiku, huku unajaribu kumsaidia mtu fulani, labda hupati hata hela kwake, bali yote ni sawa. Nikasema, "Yesu alisema katika Maandiko, 'Heri wenye rehema, maana watapata rehema.'" Na hilo ni kweli.

28 Na usiku wa leo tunataka kuliweka kanisa, katika masomo haya matatu, Mungu akiruhusu, jinsi gani na tutazamie nini, kile tulicho sisi. Tutaanzia kwenye sura ya kwanza ya Kitabu cha waraka wa Paulo kwa Waefeso. Nasi tutachukua zile sura za kwanza tatu katika masomo yetu matatu yafuatayo, tukijaribu kupata sura moja kwa jioni moja, tukiweza. Usiku wa leo, Jumatano, na Jumapili ijayo asubuhi. Waefeso, sura ya kwanza. Sasa tunaposoma pamoja, ningetaka kusema hili, ya kwamba Kitabu hiki cha Waefeso kinalingana kabisa na Kitabu cha Agano la Kale cha Yoshua. Waefeso, Kitabu cha Waefeso.

29 Sasa, kumbukeni, kama ikitokea kwamba tumeenda nje kidogo, na mafundisho yenu, mtusamehe tu na kuvumiliana nasi kwa muda kidogo. Kabla ya kukifungua, hebu na tumwombe Yeye atusaidie, tunapoinamisha vichwa vyetu.

30 Bwana, tunayakaribia Maandiko Yako matakatifu na yaliyo wakfu, ambayo ni imara kuliko mbingu zote na nchi. Kwa kuwa tunasoma katika Neno hili, linaloitwa Biblia, ya kwamba "Mbingu na nchi pia zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Basi, kwenye saa hii yenye uchaji ambayo nimekuja kwenye mimbara hii usiku wa leo, mbele ya walionunuliwa kwa Damu Yako, hawa wanadamu wapenzi na wa thamani walioketi hapa usiku wa leo, wakishikilia kwenye kila tumaini dogo wawezalo, kushikilia kwa ajili ya ile Nuru itakayokuja. Na itosheleze kabisa, usiku wa leo, ili kwamba kila mwaminio hapa ataona mahali pake, na kila mtu ambaye hajaja kwenye ushirika

huu mkuu, atakazana kwenye Ufalme, Bwana, na kubisha mlangoni hata Bawabu afungue mlango. Tujalie, Bwana.

31 Tunasoma hapa ambapo Biblia hii si ya kufasiriwa apendavyo mtu fulani. Ee Mungu, usiruhusu kwamba mimi mtumishi Wako au mtumishi yeyote mwingine atajaribu kamwe kuweka tafsiri zao wenyewe kwenye Neno. Hebu na tulisome tu na kuliamini, vile lilivyoandikwa. Na zaidi sana sisi wachungaji wa makundi ya kondoo, sisi wachungaji ambao siku moja tutakusanyika kule ng'ambo katika Nchi ile tukufu pamoja na makundi hayo madogo, nasi tutasimama katika Uwepo wa Bwana Yesu na tutaona kizazi hicho kikija, cha Paulo, na cha Petro, na cha Luka, na Marko, na Mathayo, na hao wote, na kuwaona wakihukumiwa pale pamoja na makundi yao. Mungu, jalia kwamba naweza kuweka vito milioni kumi miguuni Pako huku nikitambaa kwa unyenyekevu kuja na kuweka mikono yangu juu ya miguu Yako ya thamani, na kusema, "Bwana, hao ni Wako."

32 Ee Mungu, tujaze upya kwa Roho Wako, na kwa upendo Wako na wema Wako. Na tujalie, kama yule mshairi alivyoeleza katika ule wimbo miaka mingi iliyopita, "Mpenzi Mwana-Kondoo anayekufa, Damu Yako ya thamani daima haitapoteza nguvu zake, hata Kanisa lote lililokombolewa la Mungu limeokolewa lisitende dhambi tena. Na tangu wakati huo, kwa imani, nilipoona kile kijito kilichobubujika kutoka kwenye jeraha Lako; upendo wa ukombozi ndio umekuwa wimbo wangu, na utakuwa hivyo hata nitakapokufa. Basi katika wimbo ulio bora na mtamu," anaendelea kusema, "Nitaimba nguvu Zako za kuokoa; wakati maskini ulimi huu wenye kitembe na kigugumizi utakaponyamaza kaburini." Ndipo, kaburi halishikilii kifo chochote kwa watoto Wako. Ni mahali tu pa kupumzikia, ama mahali pa kujificha, ambapo huu uharibikao utavaa kutokuharibika.

33 Tujalie usiku wa leo kuona jambo hili, Bwana, dhahiri, kama tulivyopewa katika Neno. Tupe ufahamu. Na utuweke, Bwana, katika mahali petu pa kazi, ili tutumike kwa uaminifu hata utakapokuja Wewe. Tunaomba haya katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

34 Sasa, Kitabu cha Waefeso, kama tu nilivyokuwa nikisema, mimi . . . kwa maoni yangu, ni moja ya Vitabu muhimu sana vya Agano Jipya. Kinatuachia, mahali ambapo Ukalvini unaegemea katika tawi moja, na Uarmenia unaegemea kwenye tawi hilo lingine, lakini Kitabu cha Waefeso kinayavuta yote pamoja na kuliweka Kanisa mahali pake.

35 Sasa, nimekifananisha na Yoshua. Kama ulitambua, Israeli walipandishwa kutoka Misri, na kuna hatua tatu za safari yao. Hatua moja, ilikuwa kutoka Misri. Hatua ya pili, ilikuwa jangwani. Na hatua iliyofuatia, ilikuwa Kanaani.

36 Sasa, Kanaani haiwakilishi ule wakati wa Utawala wa Miaka Elfu. Inawakilisha tu wakati wa mshindi, majira ya kushinda, kwa sababu katika Kanaani waliua na kuchoma moto na kuiteka miji. Na hakutakuweko na kifo katika ule Utawala wa Miaka Elfu.

37 Lakini jambo lingine ambalo hilo linafanya, linaleta kuhesabiwa haki kwa imani, baada ya wao kumwamini Musa na wakatoka Misri. Kutakaswa, kule kufuata chini ya ile Nguzo ya Moto na upatanisho wa yule mwana-kondoo wa sadaka kule jangwani. Na kisha kuingia katika nchi iliyokwisha ahidiwa.

38 Sasa, ni nchi gani iliyoahidiwa mwaminio wa Agano Jipya? Ahadi ni Roho Mtakatifu. "Hata itakuwa katika siku za mwisho," Yoeli 2:28, "ya kwamba nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri. Na juu ya watumishi Wangu wa kike na wajakazi Wangu nitamwaga Roho Yangu, nao watatabiri. Nitaonyesha maajabu katika mbingu juu. Na katika nchi, nguzo za moto, na moshi, na mvuke." Naye Petro akasema, kwenye Siku ya Pentekoste, baada ya kuchukua somo lake na kuhubiri, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo," kuondoa, kusamehe, kuondolea mbali makosa yote ya huko nyuma.

39 Je, mlitambua, Yoshua, kabla wao hawajavuka Yordani, Yoshua alisema, "Piteni katikati ya kambi mkafue nguo zenu na kila mmoja wenu ajitakase, na mtu yeyote asimkaribie mkewe, kwa kuwa mnamo siku tatu mtaona Utukufu wa Mungu." Mnaona? Ni—ni tendo la kujitayarisha kuirithi ile ahadi. Sasa, ahadi kwa Israeli, ilikuwa, Mungu alimpa Ibrahimu ahadi ya ile nchi, ya Palestina, na ilipaswa kuwa mali yao milele. Nao walipaswa daima kudumu katika nchi hii.

40 Sasa, wao walipitia hatua tatu, kuingia katika nchi hii ya ahadi. Sasa angalia, jambo hili limeonyeshwa kwa mfano kamili katika Agano Jipya.

41 Sasa jambo hili, kama nilivyokwisha kusema, linapingana na baadhi ya mawazo yenu. Baadhi yenu enyi Wanazarayo wa thamani, Church of God, na kadhalika, msiache liwaudhi, bali liangalieni tu kwa makini na mwangalie mifano yake. Tazameni mwone kama kila mahali hapatimiliki kikamilifu kabisa.

42 Kulikuweko na hatua tatu za ile safari, na kuna hatua tatu za safari hii. Kwa kuwa, tunahesabiwa haki kwa imani, tukimwamini Bwana Yesu Kristo, tukiiacha nchi ya Misri, tukatoka. Na kisha tunatakaswa kwa toleo la Damu Yake, tukaoshwa na dhambi zetu, ndipo tunakuwa wasafiri na wageni, tukikiri kwamba tunaitafuta nchi, mji ujao, ama ahadi.

43 Ndivyo ilivyokuwa kwa Israeli jangwani, wageni, hawana mahali pa kupumzika, wakisafiri usiku baada ya usiku,

wakiifuata ile Nguzo ya Moto, lakini hatimaye wakaifikia ile nchi ya ahadi ambamo walikaa.

44 Hapo ndipo mwaminio ajapo. Yeye kwanza hufikia ambapo anatambua kwamba ni mwenye dhambi; ndipo anatenganishwa kwa maji, kusafishwa kwa maji, kwa Damu, na . . . au kusafishwa kwa maji katika Neno, hasa, akimwamini Bwana Yesu Kristo. Ndipo, akiisha kuhesabiwa haki kwa imani, anakuwa mshiriki, na ana amani na Mungu, kwa njia ya Kristo, amebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kumwingiza katika safari. Mnalipata? Kuingia safarini! Ndipo anakuwa mgeni na msafiri. Yuko safarini akielekea wapi? Ahadi aliyotoa Mungu.

45 Israeli walikuwa bado hawajaipokea ile ahadi, bali walikuwa safarini mwao. Na bila kuinua . . . Tafadhali mwelewe. Hapo ndipo ninyi, Wanazarayo na Wapilgrim Holiness, na kadhalika, mlipoangukia. Kwa sababu, Israeli, walipofika mahali paitwapo Kadeshi-Barnea, wakati wale wapelelezi walipovuka kule na kusema, "Nchi hiyo ni nzuri sana," lakini baadhi yao walirudi wakasema, "Hatuwezi kuitwaa, kwa sababu miji hiyo ina kuta, na kadhalika." Bali Yoshua na Kalebu wakajitokeza, wakasema, "Tunaweza kuitwaa bila shaka!" Kwa sababu ya matamshi yao ambayo tayari yameandikwa na kutiwa sahihi, wao waliamini katika kazi mbili za neema, kuhesabiwa haki na kutakaswa, wala hawangeweza kupiga hatua zaidi. Basi, sikilizeni, kizazi hicho chote kiliangamia jangwani. Ila wale wawili walioingia katika nchi ya ahadi na wakaleta ushuhuda kwamba ilikuwa ni nchi nzuri, "nasi tulikuwa tunaweza kuitwaa bila shaka, kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Mungu." Ndipo badala ya watu kusonga mbele, kumpokea Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, kupokea nguvu za Mungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ishara, maajabu, miujiza, walijisikia ya kwamba itayavunja mapokeo yao ya mafundisho. Na ilikuwaje kwake? Wakaangamia nchini! Hiyo ni kweli.

46 Bali walio waumini, hao akina Kalebu na Yoshua, waliokuwa wanaelekea kwenye ahadi, walisonga mbele kuingia kwenye nchi hiyo, wakaitwaa hiyo nchi, na wakakaa humo nchini, kama milki yao. Nasi kamwe hatukomei kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa. Na tupige hatua hadi kufikia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tusikome kwenye kumwamini Bwana Yesu, kubatizwa. Tusikome eti kwa sababu Yeye alitusafisha na maisha ya dhambi. Lakini sasa tulikaza mwendo kufikia mahali fulani, kufikia ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

47 Kwa hiyo, Waefeso hapa inatuweka kama Yoshua, mahali petu. Unaona, Yoshua, baada ya kuivuka nchi, na kuitwaa nchi, ndipo akaigawanya nchi. "Efraimu *hapa*, Manase *hapa,* na huyu *hapa,* Gadi *hapa,* Benyamini *hapa*." Akaigawanya nchi.

48 Basi tazama! Loo, hili linachoma tu mioyo yetu! Kila mmoja wa hao mama wa Kiebrania, wakiwazaa hao watoto, alitaja hasa mahali pale, katika utungu wake wa kuzaa, ambapo wao watawekwa katika nchi hiyo ya ahadi. Loo, ni somo kubwa sana! Laiti tungaliliingilia kindani, jambo ambalo lingechukua masaa kadha wa kadha. Siku moja tutakapolimaliza kanisa letu, ningetaka tu kuja na kuchukua mwezi mzima au miwili, nikae tu moja kwa moja katika hilo. Tazama wakati hao, kila mmoja wa hao akina mama, alipoita kwa sauti, "Efraimu," wakati alipokuwa katika utungu wa kuzaa, alimweka mahali pake ambapo miguu yake ilikuwa imewekwa kwenye mafuta. Mahali hasa alipokuwa kila mmoja wao!

49 Naye Yoshua, bila kujua jambo hili, ila kwa uvuvio, akiongozwa na Roho Mtakatifu, baada ya kuwa katika nchi ya ahadi, alimpa kila mmoja ahadi yake, kile hasa Roho Mtakatifu aliahidi katika kuzaliwa kule nyuma.

50 Jinsi ambavyo Mungu ameweka wengine kanisani, kwa utungu wa kuzaa! Loo, unakuwa wa kutisha sana wakati mwingine. Wakati kanisa linapougua katika mateso ya ulimwengu wa nje, likimwamini Bwana Yesu, kwamba ile ahadi ya Roho Mtakatifu ni halisi tu kwetu kama ilivyokuwa kwa Pentekoste, jinsi wanavyougua na kulia katika utungu wao wa kuzaa! Bali wanapozaliwa, na kuzaliwa mahali pao katika Ufalme wa Mungu, ndipo Roho Mtakatifu ameweka kanisani, wengine mitume, wengine manabii, wengine waalimu, wengine wachungaji, wengine wainjilisti. Kisha Yeye anawapa mle ndani, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, maarifa, hekima, karama za kuponya, aina zote za miujiza.

51 Mahali lilipo kanisa. . .Sasa hili ndilo kusudi langu la kufanya jambo hili. Kanisa daima linajaribu kuchukua kisehemu cha mtu mwingine. Lakini usifanye hivyo. Huwezi ukalima mahindi katika kisehemu cha Efraimu, iwapo wewe ni Manase. Huna budi kuchukua mahali pako katika Kristo, chukua mahali pako. Loo, linakuwa na kilindi na kukolea tunapoingia hapa, jinsi ambavyo Mungu anamweka mmoja kanisani kunena kwa lugha, mwingine. . .Sasa, tumefundishwa mara nyingi, "sote yatupasa kunena kwa lugha." Hilo ni kosa. "Sote tunapaswa kufanya hilo." La, hatupaswi. Wote hawakufanya jambo lile lile. Kila mmoja alikuwa . . .

52 Kila mmoja, ardhi ilitolewa na kugawanywa kwa uvuvio. Na, kila mmoja, ningeweza kuchukua Maandiko na kuwaonyesha jambo hilo kikamilifu, ya kwamba yeye aliwaweka mahali walipopaswa kuwa, mahali pao, jinsi ambavyo yale makabila mawili na nusu yalipaswa kuishi upande ule mwingine wa mto, jinsi ambavyo mama zao walipaza sauti wakisema jambo hilo katika kuzaliwa kwao, na jinsi ambavyo kila mahali palipaswa kuwa.

53 Na sasa baada ya wewe kuingia ndani, hilo halimaanishi kwamba uko huru na vita. Bado huna budi kupiga vita kwa kila inchi ya ardhi unayokanyaga. Kwa hiyo, unaona, Kanaani haikuwakilisha Mbingu kuu, kwa sababu ni vita na shida na mauaji na kupigana, na kadhalika. Ila iliwakilisha jambo hili, kwamba lazima uwe mwenendo mkamilifu.

54 Hapo ndipo kanisa linapokosea leo, katika mwenendo huo. Je, wajua ya kwamba hata tabia yako mwenyewe inaweza kumtupa mtu mwingine nje ya kuponywa? Tabia zenu mbaya, za dhambi zenu ninyi waaminio zisizotubiwa, zinaweza kusababisha kushindwa vibaya kabisa kwa kanisa hili. Na kwenye Siku ya Hukumu utawajibika kwa kila sehemu yake. "Loo," unasema, "sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham." Vema, hiyo ni Kweli. Liwazie hilo!

55 Yoshua, baada ya kuvuka akaingia katika ile nchi, Mungu alimtolea ahadi ya kwamba...Hebu wazieni tu, kupigana kwenye vita hivyo vyote bila ya kumpoteza mtu, bila hata kupata mkwaruzo, bila kuhitajika kuwa na nesi, au huduma ya kwanza au bendeji. Amina. Mungu alisema, "Hiyo nchi ni yenu, nendeni mkapigane." Wazieni, kupigana vita, na hakuna Msalaba Mwekundu popote hata, hakuna atakayeumia kamwe!

56 Nao wakawaua Waamori na Wahiti, bali hakuna aliyeumia miongoni mwa yeyote wao hata dhambi ilipoingia kambini. Basi wakati Akani alipotwaa lile vazi la Babeli na ile kabari ya dhahabu, na kuvificha chini ya kambi yake, ndipo kesho yake wakapoteza watu kumi na sita. Yoshua akasema, "Simama! Simama! Ngojeni kidogo, kuna kasoro! Kuna kasoro hapa. Tutaitisha siku saba za kufunga. Mungu alitupa ahadi, 'Hakuna kitakachotudhuru.' Adui zetu wataanguka miguuni petu. Na kuna kasoro hapa. Jambo fulani limeenda kombo mahali fulani, maana tuna maiti za watu kumi na sita zilizolala hapa. Wao ni ndugu zetu Waisraeli, nao wamekufa."

57 Mbona wamekufa, watu wasio na hatia? Kwa sababu mtu mmoja alienda kando ya njia. Mnaona ni kwa nini jambo hili linapaswa kufundishwa? Kanisa likijiweka sawa, likijiweka sawa na Neno la Mungu, likijiweka sawa na Mungu na kujiweka sawa mmoja kwa mwingine, wakienenda kikamilifu kabisa, kwa kiasi, mbele za watu wote, wakimcha Mungu. Kwa kuwa mtu mmoja aliiba vazi, na kutenda jambo asilopaswa kutenda, watu kumi na sita wakauawa! Nafikiri walikuwa kumi na sita, labda wengi zaidi. Naamini walikufa watu kumi na sita.

58 Yoshua akapaza sauti, kasema, "Kuna kasoro! Mungu alitoa ahadi, na kuna kasoro."

59 Wakati tunapowaleta wagonjwa mbele zetu, na wasiponywe, tunahitaji kuitisha kufunga kwa uchaji, tuitishe mkutano. Kuna kasoro mahali fulani. Mungu alitoa ahadi, Mungu hana budi kushikilia hiyo ahadi, naye ataitekeleza.

60 Naye akaagiza kufunga. Ndipo wakagundua, wakapiga kura. Naye Akani akakiri jambo hilo. Nao wakaiua jamaa ya Akani na kila kitu, na kuyateketeza majivu yao, na wakayaacha hapo kama ukumbusho. Ndipo Yoshua akaendelea moja kwa moja na vita, akitwaa kila kitu, bila mkwaruzo wala jeraha. Haya basi.

61 Siku moja alikuwa anahitaji muda kidogo, muda zaidi. Jua lilikuwa linatua, hao watu hawangeweza kupigana vizuri sana usiku. Yoshua, yule shujaa maarufu, aliyetiwa mafuta na Mungu, aliyewekwa mahali pake nchini, kama vile Waefeso kwa Kanisa jipya, limiliki, lilimiliki, likimiliki nchi, kuitwaa. Yeye alihitaji muda kidogo, kwa hiyo akasema, "Ewe jua, simama!" Nalo likasimama kwa yapata masaa kumi na mawili, hata alipoitwaa ile nchi. Mnaona?

62 Sasa Kitabu cha Waefeso kinatuweka katika nafasi katika Kristo, jinsi walivyokuwa katika Nchi Takatifu. Tunawekwa mahali petu si katika Nchi Takatifu, bali katika Roho Mtakatifu! Sasa hebu tusome Neno moja tu, tuone jinsi kanisa lilivyo kamilifu:

> *Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, . . .*

63 Loo, napenda hilo! Mungu alimfanya mtume. Hakuna wazee waliomwekea mikono, hakuna maaskofu waliomtuma popote, bali Mungu alimwita na kumfanya mtume.

> *Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu* (waliotakaswa) *walioko Efeso, na kwa wanaomwamini* Yesu Kristo:

64 Angalia jinsi yeye anavyoandika haya. Haya si kwa wasioamini. Haya ni kwa kanisa. Haya yanaagiziwa walioitwa, hao waliotakaswa na kuitwa walio katika Kristo Yesu.

65 Sasa, ukitaka kujua jinsi tunavyoingia katika Kristo Yesu, kama utafungua Wakorintho wa Kwanza 12, ilisema, "Kwa maana kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Vipi? Kubatizwa kwa nini? Roho Mtakatifu. Si kwa ubatizo wa maji, enyi watu wa Kanisa la Kristo, bali kwa R-o-h-o mmoja wa herufi kubwa, kwa Roho mmoja. Si kwa kupeana mkono kumoja, kwa barua moja, si kwa kunyunyiziwa kumoja. Bali, "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili mmoja," milki yetu, ile nchi aliyotupa Mungu tupate kuishi ndani, Roho Mtakatifu. Kama vile tu alivyowapa Wayahudi Kanaani, Yeye ametupa Roho Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Mnalipata?

66 Sasa, Yeye anawazungumzia Wakanaani wa kiroho, Israeli, Israeli wa kiroho ambao wameimiliki ile nchi. Loo, hivi wewe huna furaha kwamba umetoka kwenye vitunguu saumu vya Misri? Hivi huna furaha ya kwamba umetoka jangwani? Isitoshe, kumbuka, iliwabidi kula mana, chakula cha Malaika kilichotoka

Mbinguni, mpaka walipoingia kwenye hiyo nchi. Na walipovuka kuingia katika nchi hiyo, mana ikaacha kuanguka. Walikuwa wamekomaa kabisa wakati huo, nao wakala mahindi ya zamani ya nchi hiyo. Basi, sasa kwa kuwa ninyi si watoto wachanga tena, sasa kwa kuwa hamtamani maziwa ya akili yasiyoghoshiwa ya Injili, kwamba si lazima mbembelezwe kitoto, na kupigwapigwa mgongoni, na kushawishiwa kuja kanisani, sasa kwa kuwa ninyi ni Wakristo waliokomaa kikamilifu, mko tayari kula nyama ngumu sasa. "Mko tayari kufikia kitu fulani," yeye alisema. Mko tayari kufahamu kitu chenye kilindi na kinono. Loo, tutakifikia hicho moja kwa moja. Na, loo, kimefichwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. Yeye alisema, "Sasa kwa kuwa mmefikia jambo hili, ninawaandikia ninyi haya." Si kwa wale ambao ndio kwanza watoke Misri, si kwa wale wangali safarini bado, bali kwa wale walio katika nchi ya ahadi, ambao wamepokea ile ahadi.

67 Wangapi wamepokea ahadi ya Roho Mtakatifu? Loo, hivi hamna furaha kwamba mko katika nchi hii? Hapa sasa, mkila mahindi ya zamani, mkila vitu imara vya Mungu na mna ufahamu dhahiri. Nia ze—zenu za roho hazijachafuliwa. Mnajua yakini Yeye ni Nani. Mnajua yakini kile Yeye alicho. Mnajua yakini mnakoelekea. Mnajua habari Zake zote hasa. Mnamjua mliyemwamini na kusadiki ya kwamba Yeye aweza kukilinda kile mlichoweka amana Kwake hata siku ile. Loo, huyo ndiye, huyo ndiye ambaye Paulo anamzungumzia sasa. Sikiliza kwa makini. Sasa tazama.

. . .wanaomwamini Kristo Yesu:

68 Sasa, hebu nilifanye kanisa kurudia hayo. Tunaingiaje katika Kristo? Kwa kujiunga na kanisa? La. Kwa kuandika jina letu katika kitabu fulani? La. Kwa kubatizwa kwa kuzamishwa katika maji mengi? La. Tunaingiaje katika Kristo? Kwa Roho Mtakatifu mmoja sote tumebatizwa katika ahadi moja, ule Mwili, nasi ni washiriki wa kila kitu cha hiyo nchi. Amina! Loo, na—napenda hilo. Kama sikuwa nimepwelewa na sauti, ningalipaza sauti. Jamani, niingiapo katika nchi hii, ni yangu. Niko nyumbani sasa; mimi niko Kanaani. Niko radhi kwa chochote Mungu anachotaka kunitumia kwa ajili yake. Mimi ninatembea katika nchi takatifu, mwana wa Mfalme, tayari nimevalishwa joho na niko tayari. Nimetoka Misri, nikaja kupitia nchi ya ahadi, nikastahimili majaribu, nikavuka Yordani nikaingia katika ahadi hii iliyobarikiwa. Loo, nilipataje jambo hilo? Kwa Roho mmoja. Jinsi ile ile Paulo alivyoipata, ikatenda juu yangu vile vile ilivyotenda juu yake, jinsi ile ile ilivyotenda juu yako. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa." Si kunyunyiziwa, nyunyizo moja tu Lake, unajisikia vizuri sana; bali kuzamishwa ndani! Wote wanapaswa kuzamishwa, katika Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo ahadi.

69 Waefeso wetu, Yoshua wetu, ambaye ni Roho Mtakatifu, *Yoshua* maana yake ni "Yesu, Mwokozi." Yoshua likimaanisha Roho Mtakatifu akiwakilisha hilo katika kiroho kama vile hilo lilivyofanya katika mambo ya kawaida, ya kwamba Yeye ndiye Shujaa wetu mkuu. Yeye ndiye Kiongozi wetu mkuu. Kama vile Mungu alivyokuwa pamoja na Yoshua, ndivyo Mungu (katika Roho Mtakatifu) anavyotuongoza kila mahali. Na dhambi inapoingia kambini, Roho Mtakatifu huagiza kusimama, "Kuna shida gani humu kanisani? Kuna kasoro." Loo, hivi hamwezi kuona jinsi tulivyo na wana wengi mno wa Kishi sasa? Sauli wengi kupita kiasi wakitokea seminari na shule za theolojia na kuenda huko nje na kufundisha mambo haya ya upotovu, kama vile Biblia ilivyosema wangefanya. "Inavyoonekana, bila kuwa na ile Imani, wakijitenga nanyi, bila ushirika nanyi, na kadhalika, wakiwa na mfano wa utauwa huku wakikana Nguvu zake, hao nao mjiepushe nao." Hawajui wanakotoka, hawawezi kutoa sababu yoyote.

70 Nasema jambo hili kutoka kwa Ndugu Booth Clibborn, rafiki yangu, kama kuna chochote ambacho ni ha-. . .haramu na kisichoumbwa na Mungu, chochote kile ulimwenguni, ni nyumbu. Nyumbu ndicho kitu kilicho duni kuliko vyote. Yeye ni. . .ha—hajui yeye ni nini. Hawezi kujizaa mwenyewe tena. Nyumbu hawezi kujizalisha kwa nyumbu mwingine na kuwa nyumbu. Amekwisha. Hajui baba yake alikotoka, wala hamjui mamaye, kwa kuwa yeye ni maskini—maskini punda na farasi jike. Mungu hakufanya hivyo kamwe. Usimsingizie Mungu kitu kama hicho. Mungu hakufanya hivyo kamwe. Mungu alisema, "Kila kitu kitazaa kwa jinsi yake." Naam, bwana. Bali nyumbu ni—ni. . .baba yake alikuwa punda na mamaye alikuwa farasi jike, kwa hiyo hajui yeye ni wa upande gani. Yeye—yeye—yeye ni farasi anayejaribu kuwa nyumbu, au nyumbu. . . au—au ni farasi anayejaribu kuwa punda, punda anayejaribu kuwa farasi. Hajui yeye ni wa upande gani. Naye ni kitu chenye kichwa kigumu kuliko vyote kilichoko ulimwenguni. Huwezi ukamwamini hata kidogo.

71 Na hivyo ndivyo walivyo watu wengi kanisani. Hawajui baba yao ni nani, hawajui mama yao ni nani. Jambo pekee wajualo, wao ni Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti, au Wapentekoste, au chochote kile. Hawajui wanakotoka. Na maskini punda, unaweza kumpigia kelele jinsi unavyotaka kumpigia kelele, naye atasimama hapo na kuinua hayo masikio makubwa, na kutazama. Unaweza ukawahubiria usiku kucha, nao hawajui cha zaidi kidogo walipoondoka kuliko walivyojua walipoingia. Sasa, hilo ni kweli kabisa. Sikusudii kuwa fidhuli, bali nataka kuwaambia Kweli.

72 Ila kuna jambo moja wanaloweza kufanya, wao ni wafanyakazi wazuri. Loo, wao wanafanya tu kazi, kazi, kazi, kazi. Hilo linanikumbusha juu ya kundi la hawa Waarmenia

ambao daima wanajaribu kwa jitihada zao kuingia Mbinguni. Hiyo ni kweli, nyumbu. Loo, Shirika la Huduma ya Wanawake, na mlo wa jioni wa nyama ya kuku, kwa ajili ya mshahara, wa mhubiri. "Na hatuna budi kuwa na dansi hili, na tamasha hii." Ni kazi, kazi, kazi, kazi, kazi, kazi, kazi tu. Na, wao, wanafanya kazi ya nini?

73 Hebu waulize, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

74 Wao wananyosha maskio yao, na hawajui wao ni wa wapi, "Una maana gani? *Haya* yote yalitoka wapi? Una maana gani, Roho Mtakatifu? Sijasikia kitu chochote juu Yake. Loo, hapana shaka wewe ni namna fulani ya mshupavu wa dini." Unaona, hawajui baba yao alikuwa nani, ama mama yao alikuwa nani, hata. Nawe huna budi kuwapiga kwa kila kitu ufanyacho, unapiga *hapa* na kupiga *pale*, na kupiga *hapa* na kupiga *pale*. Hiyo ni kweli, nyumbu mzee.

75 Lakini, nakwambia, haikubidi kufanya hivyo kwa farasi mwenye asili bora. Kwatua tu mjeledi mara moja juu yake, na, ndugu, huyo ameondoka. Anajua anachofanya. Loo, ni vizuri jinsi gani kumpanda mwenye asili bora! Ni vizuri jinsi gani kusema, "Njoo, jamani." Loo, jamani, afadhali ujishikilie vizuri, atayaacha matandiko hewani.

76 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Wakristo wenye asili bora. Haleluya! "Pokeeni Roho Mtakatifu. Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu." Wameenda, upesi tu wawezavyo kuyafikia maji, wameenda. Hawawezi kupumzika mchana na usiku mpaka wampokee Roho Mtakatifu. Kwa nini? Mnajua, Mkristo anajua Baba yake alikuwa nani. Mnaona, inahitaji wawili kuzaa mtoto. Hiyo ni kweli, baba na mama. Nyumbu hajui baba alikuwa nani, wala mama alikuwa nani. Lakini sisi tunajua Baba na Mama alikuwa Nani, kwani tulizaliwa kwa Neno lililoandikwa la Mungu, lililothibitishwa na Roho. Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Kama mkitubu na kubatizwa, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

77 Isitoshe, ndugu, Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, (loo, jamani) roho yake, mara anapolipata Neno, anampokea Roho Mtakatifu. Mwulize jambo fulani wakati huo! Anajua anakosimama. "Unaamini katika uponyaji wa Kiungu?"

"Amina!"

"Unaamini katika Kuja kwa Pili?"

"Amina!"

78 Mwulize nyumbu jambo hilo. Dini ya nyumbu, "Ah, sijui. Daktari Jones alisema wakati mmoja . . ." Aha! Basi, shika njia

ukamfuate Sauli. Unaona? “Loo, hawajui. Vema, nakwambia, kanisa langu halina uhakika nalo.”

79 Loo, ndugu, lakini mwanamume na mwanamke aliyezaliwa mara ya pili ana uhakika tu wa kule kuja kwa Bwana Yesu, wana uhakika tu wanaye Roho Mtakatifu kama kulivyo na Roho Mtakatifu wa kutolewa.

80 Sasa, Yesu alisema . . . Yule mwanamke kisimani, “Sisi huabudu katika mlima huu, nao Wayahudi wanaabudia Yerusalemu.”

81 Yeye akasema, “Mwanamke, yasikie Maneno Yangu! Saa yaja, na sasa ipo, ambapo Baba anawatafuta hao watakaomwabudu katika Roho na Kweli.”

82 “Neno Lako ni Kweli.” Na kila mtu atakayesoma Biblia na kuamini kila Neno ambalo Biblia inasema, na kufuata maagizo Yake, na kumpokea Roho Mtakatifu yeye yule ambaye walimpokea, jinsi ile ile walivyompokea, matokeo yale yale waliyopata Kwake, nguvu zile zile walizopata walipompokea, anajua Baba yake na Mama yake walikuwa nani. Anajua amesafishwa katika Damu ya Yesu Kristo, akazaliwa na Roho, akajazwa na upako wa Mungu. Anajua anaposimama. Hakika! Yuko Kanaani. Anajua alikotoka. Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. Hebu mwulize, “Je, umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?”

“Amina, Ndugu!”

83 Nilipokuwa nimesimama hivi majuzi karibu na mzee mtakatifu, mwenye umri wa miaka tisini na miwili, nikizungumza na mchungaji wake mwenye umri wa miaka themanini, nikasema, “Nyanya?”

Akiwa amechangamka kabisa, alisema, “Ndiyo, mwanangu.”

84 Nikasema, “Imekuwa muda gani tangu ulipompokea Roho Mtakatifu?”

Akasema, “Mungu atukuzwe! Nilimpokea yapata miaka sitini iliyopita.”

85 Sasa, kama yeye angalikuwa nyumbu, angalisema, “Sasa, ngoja kidogo, nilipewa kipaimara na kunyunyiziwa maji nilipokuwa . . . Vema, bila shaka, nao wakanipeleka kanisani nami nikapeleka barua yangu kwa *nanii*.” Loo, nirehemu! Hata hawajui wao ni wa wapi.

86 Bali yeye anajua ilikotoka haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Alikuweko lilipotukia. Alizaliwa kwa maji na kwa Roho. Alijua, na maji kwa kuoshwa kwa maji katika Neno, inahitaji Neno.

87 Sasa tazama jinsi hili lilivyoandikwa, “Kwa wale walio katika Kristo Yesu.” Paulo, sasa, kumbuka . . . Ninachukua muda mrefu, bali sitaimaliza sura hii. Lakini nitaharakisha . . .

Mnalipenda? Loo, linatuambia mahali tulipo, lakini hatuwezi kufanya hivyo katika usiku mmoja tu. Tunahitaji mwezi mmoja au miwili katika jambo hili, kila usiku, kulipitia lote, Neno kwa Neno. Kurudi nyuma na kulileta katika historia na kulieleza waziwazi, Neno kwa Neno, na kuwaonyesha kwamba ni Kweli. Sasa hebu nisome kifungu hicho upesi tena.

> *Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu* (si mapenzi ya mwanadamu), *kwa watakatifu walioko Efeso, na* (kiunganishi) *kwa wanaomwamini Kristo Yesu:*

88 Inamaanisha, "Wamekwisha itwa watoke, wakatengwa, na sasa wamekwisha batizwa kwa Roho Mtakatifu, nao wako katika Kristo Yesu. Ninawaandikia barua hii, enyi wapendwa wangu." Loo! Nawaza juu ya Paulo pale pamoja nao sasa hivi, loo, furaha jinsi gani! Maskini mtume huyo mzee alikatwa kichwa chake kule chini. Nilisimama karibu na mahali walipomkata kichwa. Lakini, loo, kichwa chake kiko kwenye ule mwili mpya, wala hakiwezi kukatwa tena. Naye amesimama pale pamoja nao dakika ii hii, mtume yule yule aliyeandika Haya. Naye akasema, "Kwenu ninyi mlio katika Kristo Yesu! Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili huu mmoja." Sasa tazama.

> *Neema na* iwe *kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu, na . . . Bwana Yesu Kristo.*

> *Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa zote . . .*

Loo, unasikia hayo, Charlie?

> *. . . ametubariki kwa baraka zote za rohoni . . .*

89 Si kidogo tu kwa mitume, na kidogo kwa *huyu*, bali Yeye ametubariki kwa baraka zote za rohoni. Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye siku ya Pentekoste ndiye Roho Mtakatifu yeye yule hapa usiku wa leo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyemfanya Mariamu apaze sauti na kunena kwa lugha, na kuwa na wakati mzuri sana na kushangilia, na mambo yale aliyofanya, ndiye Roho Mtakatifu yeye yule hapa usiku wa leo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyemwachilia Paulo kwenye merikebu ile ya kale, ambapo ilionekana kana kwamba ilikuwa imejaa maji na imeangamia, na siku kumi na nne usiku na mchana, hakuna mwezi wala nyota. Alitazama huko nje na kila wimbi lilikuwa na pepo juu yake, akiangalia, na kutoa meno yake, na kusema, "Nitakuzamisha, maskini wee, sasa. Nimekupata sasa."

90 Na wakati Paulo aliposhuka kwenda kuomba kidogo, hapo alisimama Malaika, kasema, "Usiogope, Paulo. Merikebu hii ya kale itavunjika kwenye kisiwa fulani. Endelea na ule chakula chako cha jioni, yote ni shwari sasa."

91 Huyu hapa anakuja na hiyo minyororo kwenye maskini mikono yake midogo, akiikokota kwa miguu yake, na akasema, “Msiogope, enyi wanaume, kwa kuwa Mungu, Malaika wa Mungu, ambaye mimi ni mtumishi wake, alisimama mbele yangu akasema, ‘Paulo, usiogope.’” Roho Mtakatifu yuyo huyo yuko hapa usiku wa leo, Roho yule yule wa Mungu, akituhudumia baraka zile zile za rohoni.

> *. . .aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho . . .*

92 Loo, hebu tusimame dakika moja tu zaidi hapa. “Mahali pa Mbinguni.” Sasa, si popote pale, bali mahali pa Mbinguni. Tumekusanyika katika “Mbingu,” ina maana kwamba hapo ndipo mahali pa mwaminio. Basi, kama nimeomba vya kutosha, nawe umeomba vya kutosha, au kanisa limeomba vya kutosha, na tuko tayari kwa Ujumbe, nasi tumekusanyika pamoja kama watakatifu, walioitwa wakatoka, waliobatizwa na Roho Mtakatifu, wamejazwa na baraka za Mungu, wameitwa, wakateuliwa, wameketi pamoja mahali pa Mbinguni sasa, sisi ni wa Kimbinguni katika nafsi zetu. Roho zetu zimetuleta katika hali ya Kimbinguni. Loo, ndugu! Haya basi, hali ya Kimbinguni! Loo, nini kingetokea usiku wa leo, kungetokea nini usiku wa leo kama tungekuwa tumeketi hapa katika hali ya Kimbinguni, huku Roho Mtakatifu anatembea katika kila moyo ambao umezaliwa upya na ukawa kiumbe kipya katika Kristo Yesu? Dhambi zote zikiwa chini ya Damu, katika ibada kamilifu, huku tumemwinulia Mungu mikono yetu na mioyo yetu imeinuliwa, tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tukiabudu pamoja katika mahali pa Mbinguni.

93 Je, umewahi kuketi mahali kama hapo? Loo, mimi nimeketi hata ningelia kwa furaha na kusema, “Mungu, kamwe usiniache nikaondoka hapa.” Mahali pa Mbinguni tu katika Kristo Yesu!

94 Akitubariki na nini? Uponyaji wa Kiungu, kutangulia kujua, ufunuo, maono, nguvu, lugha, tafsiri, hekima, maarifa, baraka zote za Kimbinguni, na furaha isiyoneneka na iliyojawa na Utukufu, kila moyo umejazwa na Roho, tukitembea pamoja, tukiketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, hakuna wazo moja baya kati yetu, hakuna hata sigara moja inayovutwa, hakuna nguo moja fupi, hakuna jambo *hili*, *lile* au *lingine,* hakuna wazo moja baya, hakuna aliye na neno dhidi ya mwingine, kila mtu akizungumza katika upendo na upatanifu, kila mtu katika moyo mmoja na mahali pamoja, “ndipo kukaja ghafla toka Mbinguni uvumi kama wa upepo wa nguvu ukienda kasi.” Haya basi, “Ametubariki kwa baraka zote za rohoni.”

95 Ndipo huenda Roho Mtakatifu akashuka juu ya mtu fulani, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI. Nenda mahali fulani ukafanye jambo fulani.” Tazama jambo hilo likitendeka *hivyo* tu. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Unaona? “BWANA

ASEMA HIVI. Fanya jambo fulani mahali fulani.” Angalia likitukia jinsi *hiyo*. [Ndugu Branham anadata vidole vyake.]

96 “Ametubariki pamoja katika baraka zote za Kimbinguni mahali pa Mbinguni.” Angalia!

Kama vile alivyotuchagua . . .

97 Je, tulimchagua sisi, au alituchagua Yeye? Yeye alituchagua. Lini? Usiku ule tuliomkubali? Katuchagua!

> *Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa* misingi *ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu . . . wasio na hatia mbele zake katika . . .*(madhehebu?) . . . *katika pendo:*

98 Mungu alituchagua lini? Mungu alikuchagua lini wewe uliye na Roho Mtakatifu? Alikuchagua lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alikuona kimbele na alijua ya kwamba ungempenda. Na kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuchagua wewe, na akamtuma Yesu apate kuwa kipatanisho cha dhambi zako, akuite upate kupatanishwa, Kwake, kwa upendo. Loo, laiti tungalikuwa na muda wa dakika zingine chache.

99 Hebu basi, kabla hatujaendelea sana, turudi nyuma, Mwanzo 1:26. Nitaendelea nalo Jumatano. Mungu alipomwumba mtu . . . Kabla hajamwumba mtu, alijiita Mwenyewe “El,” E-l, El; E-l-h, “Elah,” “Elohim.” Neno hilo linamaanisha, katika Kiebrania, “aishiye peke yake,” peke Yake kabisa. Hakuna kilichokuweko kabla Yake, Ndiye kitu pekee kilichokuwepo, Yeye aishiye peke yake! El, Elah, Elohim, maana yake ni “anayejitosheleza, mwenye nguvu zote, Mwenyezi, Yeye aishiye peke yake.” Loo!

100 Lakini katika Mwanzo 2, wakati Yeye alipomuumba mtu, Yeye alisema, “Mimi ni,” Y-a-h-u, J-u-v-u-h, *Yahweh*, “Yehova.” Lilimaanisha nini? “Mimi ndimi Yule aishiye peke Yake aliyeumba kitu fulani kutoka kwangu Mwenyewe, kiwe Mwanangu, au mtoto Wangu wa muda, au mdogo.” Utukufu! Kwa nini? Yeye alimjalia mwanadamu . . . *Yehova* maana yake ni kwamba “Yeye alimjalia mwanadamu kuwa mungu mdogo.” Kwa sababu Yeye ni Mungu Baba, na Yeye alimfanya mwanadamu kuwa mungu mdogo, kwa hiyo Yeye si anayeishi peke yake tena, Yeye anaishi na familia Yake. Elah, Elah, Elohim. Naam, sasa Yeye ni Yehova. *Yehova,* likimaanisha “Yeye aishiye pamoja na familia Yake.” Sasa, Mungu alimfanya mwanadamu aitawale dunia nzima, alikuwa na milki. Na dunia ilikuwa ni milki ya mwanadamu. Hilo ni Andiko? Basi kama hiyo ni milki yake, yeye alikuwa mungu juu ya dunia. Yeye angenena, na ingekuwa hivyo. Angenena *hili,* nalo lingekuwa hivyo. Loo! Huyo hapo, Mungu, Yehova, Yule ambaye wakati mmoja aliishi katika upweke, bali sasa yuaishi pamoja na familia Yake, na watoto Wake wakiwa pamoja Naye. Haya basi.

101 Sasa, someni hayo. Tutayaingilia hayo Jumatano usiku, tutakapokuwa na muda mwingi zaidi. Tuna yapata dakika zingine kumi na tano kisha tutaninii. . .Nilidhani ningefikia mahali fulani hapa, bali hatutapafikia, kufikia ambapo tunatiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi. Vema.

102 Sasa, tuliitwa lini tuwe watumishi wa Mungu? Orman Neville aliitwa lini kuwa mtumishi wa Mungu? Loo, jamani! Hili huniduwaza. Nitawaambieni, hebu na tuchukue Maandiko machache. Nawatakeni Mfungue Petro wa Kwanza 1:20. Na, Pat, fungua Ufunuo 17:8. Nami nitafungua Ufunuo 13. Sasa tunataka kusikiliza hapa, unataka kujua ni lini Mungu alikuita kuwa Mkristo. Loo, napenda hili. Hili, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Vema, Ndugu Neville, umepata Petro wa Kwanza 1:20. [Ndugu Neville anasema, "1:20."—Mh.] Sawa, soma 1:19 na 1:20. Sikilizeni hili. ["1:19 na 20."] Ndiyo.

> [*Bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo:*]
>
> [*Naye amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia, lakini alifunuliwa mwisho wa zamani hizi kwa ajili yenu.*]

103 Yeye alijulikana lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Ndugu Pat, nisomee Ufunuo 17:8.

> [*Yule mnyama uliyemwona alikuweko, naye hayuko; naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu: na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako.*]

104 Ni nani atakayedanganywa? Ni nani atakayedanganywa na mtu huyu wa dini kama alivyodanganywa Sauli? Ambaye alikuwa mjanja sana hata ingewapoteza akina nani? Walio Wa-. . .[Kusanyiko linasema, "Wateule."—Mh.] kama. . . ["yamkini."] kama yamkini. Vema, Ufunuo 13:8, hebu niwasomeeni:

> *Na watu wote wakaao juu ya nchi wata. . .wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa* kabla ya *kuwekwa misingi ya dunia.*

105 Majina yetu yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo lini? Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Wakati Mungu alikuwa Yehova, El, Elah, Elohimu, Yeye aishiye peke yake. Kama tu Almasi moja kubwa mno, Naye asingelikuwa kitu kingine, ila ndani ya Almasi hii sifa Zake zilikuwa Mwokozi. Katika

sifa hizi, ndani Yake, alikuwa Mponya. Vema, hapakuwepo na chochote cha kuokolewa wala hapakuwepo na cha kuponywa, bali sifa Zake zilikileta hicho. Kwa hiyo, ndipo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, wakati Yeye alipojua, ya kwamba lile onyesho Lake kuu hapa ndani, ya kwamba Yeye angekuwa Mwokozi, ya kwamba angekuja na afanyike mwili na kukaa kwetu, Naye alijua kwa mapigo Yake tungeponywa, Yeye alimchinja huyo Mwana-Kondoo katika Kitabu Chake kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, na akaandika jina lako katika Kitabu hicho kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Loo!

106 Sikilizeni Hili! Kuchaguliwa kimbele huangalia nyuma kwenye kujua kimbele, namaanisha kuteuliwa. Kuteuliwa huangalia nyuma kwenye kujua kimbele, nako kujua kimbele huangalia kwenye mwisho wa safari. Msije mkasahau jambo hilo, ya kwamba kuteuliwa huangalia huku nyuma, hili hapa, "Nilikuwa gugu. Nilizaliwa katika dhambi, nikaumbika katika uovu, nikaja ulimwenguni nikisema uongo, nilizaliwa kati ya wenye dhambi. Baba na mama na jamaa yangu yote, wenye dhambi. Nilikuwa gugu. Lakini, mara, nikawa chembe ya ngano. Ilitukiaje?" Hiyo, hiyo ni nini? Uteuzi. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, aliteua kwamba hilo gugu litakuwa punje ya ngano. "Sasa najua kwamba mimi ni punje ya ngano, kwa sababu nimeokolewa. Ninafanya hivyo vipi?" Naangalia nyuma na kuona kwamba Yeye aliikusudia, zamani za kale. Kwa kutangulia kujua Yeye aliona ya kwamba mimi ningempenda, kwa hivyo akafanya upatanisho kwa njia ya Mwanawe Mwenyewe, ili kupitia Yeye nipate kutoka kuwa gugu niwe punje ya ngano. "Sasa, niko wapi sasa?" Nimeokolewa, natembea katika neema ya Mungu. "Kuchagua kimbele huangalia nini?" Kwenye mwisho wa safari. "Yeye atanipeleka wapi, na ninaelekea wapi?" Amina. Hilo limekupata. Haya basi.

107 Sasa hebu na tusome mbele kidogo, ndipo itatubidi kufunga upesi sana.

> *Kama vile*. . . alituchagua *katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, ili tuwe watakatifu*. . . *wasio na hatia mbele zake katika pendo:*
>
> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe*, kutangulia kutuchagua *ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,*

108 Yeye alifanya nini? Yeye, kwa kutangulia kujua, alituona sisi tangu zamani, akijua kwamba Yeye alikuwa Mwokozi, aliyeishi peke yake. Hapakuwepo na Malaika, hakuna chochote; ni Mungu tu, Elah, Elohimu, aishiye peke Yake, hakuna kitu ila Yeye peke Yake. Lakini ndani Yake mlikuwemo Mwokozi. Vema, ataokoa nini, hakuna kilichopotea? Akijua hivyo, basi alijua kwamba sifa hii kuu ndani Yake ingedhihirisha kitu kule

ng'ambo ambacho Yeye angeokoa. Ndipo alipotenda jambo hilo, kwa kujua tangu zamani Yeye aliangalia huku chini na akaona kila mmoja ambaye angelilikubali. Na kisha kwa kufanya hivyo, Yeye alisema, "Kuokoa hicho, njia pekee niwezayo kufanya hivyo, itakuwa ni kushuka Mwenyewe na kufanyika mwili kisha nimtwike Yeye dhambi ya mwanadamu, na amfie, kusudi Mimi nipate kuwa Ndiye wa kuabudiwa," kwa sababu Yeye ni Mungu, kitu cha kuabudiwa.

109 Basi akashuka akaja na kujitwika Mwenyewe. Na alipokuwa anafanya hivyo, Yeye alifanya hivyo kusudi apate kukuokoa wewe unayetaka kuokolewa. Unaona ninalomaanisha? Kwa kutangulia kujua, Mungu asiye na kikomo, Yeye aliyejua mambo yote, alimwona Mwana-Kondoo, Naye akamchinja huyo Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, na akaliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Naye aliona udanganyifu wa Shetani, yale ambayo angefanya. Kwa hiyo akaliandika jina lako mle. Naye akasema kwamba yule mpinga-Kristo angekuwa wa kidini sana, mzuri sana, jamaa mzuri mno, mtu mwerevu sana, mtu wa kidini sana, hata angewadanganya walio Wateule kama yamkini. Lakini haiwezekani, kwa sababu majina yao yalijulikana tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Aliwachagua kwa uteuzi, na kwa kuchaguliwa tangu zamani wao wanajua wanakoelekea. Haya basi.

110 Sasa, ni nani angeweza kulitilia jambo hilo shaka? Hivyo ndivyo alivyosema Paulo. Hayo ni Maandiko ya Paulo. Hayo ni maandishi ya Paulo. Hivyo ndivyo alivyolifundisha kanisa lake. Kanisa, mahali pake, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Wakati Mungu, katika utungu Wake wa kuzaa, alipokuwa anazaa, alipokuwa akikuzaa wewe, akijua yale ambayo ungetenda, Yeye alikuweka mahali pako katika Mwili Wake Mwenyewe, uwe mke wa nyumbani, uwe mkulima, uwe mhubiri, uwe nabii, uwe *hiki* au *kile*. Alikuweka wewe mahali pako. Ndipo tukisha toka kwenye mashamba ya vitunguu saumu ya Misri, kwa njia ya kutakaswa, na tumebatizwa tukaingizwa kwenye nchi ya ahadi . . . Kwa kuwa, ahadi ya Mungu ni Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30, inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Kisha Mungu, akishalichagua kanisa tangu zamani, Yeye alisema, "Na watu wote, kutakuwa na mamilioni mara mamilioni watakaoishi kidini sana na wawe wamedanganywa." Wale tu ambao hawatadanganywa watakuwa wale ambao wameingia katika nchi ya ahadi, ambao kabla ya kuwekwa misingi ya dunia majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, nao wameingia katika nchi ya ahadi, na wanaifurahia.

111 Watu wengi wanaogopa utafanya mambo ya kuchekesha. Watu wengi wanaogopa Roho Mtakatifu atakufanya ufanye

jambo li—litakalokuaibisha kwa watu. Watu wengi wanaogopa watalia, na wapenzi wao watawaona wakilia, au mama, au jirani yako, au bosi wako atakuona.

112 Hebu niwaambieni juu ya mtu mmoja wakati mmoja, kabla ya kufunga. Kulikuwa na mtu jina lake Daudi, na wakati sanduku la Mungu lilikuwa huko katika nchi ya Wafilisti, nalo likaja, linakokotwa na sanduku, maksai mzee alikuwa anayakokota, Daudi alipoona sanduku hilo likija, alikuwa amevaa joho dogo, akakimbia kule nje, akarusha miguu yake hewani, na kuruka huko na huko, akapaza sauti na kuruka juu, akacheza na kurukaruka na kucheza. Na, yeye, ni mfalme wa Israeli! Ndipo mkewe akaangalia dirishani akamwona akifanya mambo ya ajabu sana, akamdharau. Mbona, hapana shaka alisema, "Mpumbavu! Mwangalie kule, vile anavyofanya, akirusha miguu yake hewani, na akirukaruka na kufanya namna hiyo. Mbona, bila shaka ana kichaa!" Ndipo usiku huo alipoingia, mwanamke akasema, kwa maneno kama haya, "Mbona, umenitahayarisha. Mbona, wewe, mfalme, mume wangu, hadharani unafanya namna hiyo, unafanya hivyo!"

113 Daudi akasema, "Kesho nitafanya vyema zaidi ya hayo. Naam, bwana!" Akasema, "Hujui nilikuwa nikimchezea Bwana?" Alivuka! Alikuwa katika nchi ya ahadi. Alikuwa amepoteza mitindo yote ya kibinafsi na uchafu wa ulimwengu. Alifurahi sana kujua kwamba lile sanduku lilikuwa linakuja kwenye jiji lake mwenyewe.

114 Na, loo, nawaambieni, watu wengine wanaogopa kumpokea Roho Mtakatifu, wakiogopa kwamba huenda wakanena kwa lugha. Wanaogopa kwamba mtu fulani angesema, "Sasa, yeye ni mmoja wa hao jamaa wa lugha." Wanaogopa kuja kanisani na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu wanalionea aibu. Uh! Loo!

115 Mtu fulani alisema kwamba itanibidi kuamrisha kanda zangu zirudishwe, kwa sababu nilikuwa nimehubiri juu ya kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Sitazirudisha. Ninatengeneza zingine zaidi! Hiyo ni kweli, kwamba, ninatengeneza zingine zaidi! Hiyo ni Biblia. Kama hawapendi yale tuliyofanya jana, hebu na waangalie tutakayofanya kesho! Hilo ndilo jambo la kufanya, unaona, endelea kusonga mbele. Hapana mwisho wake, kwa sababu ni la Bwana. Ni Mungu.

116 Unajua alilofanya Mungu? Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni, akasema, "Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu." Daudi hakutahayarika. Yeye alikuwa mtumishi wa Bwana. Alimpenda Bwana. Naye alikuwa na furaha sana, amejawa furaha nyingi sana, mpaka hakuwa na habari juu ya fahari za kibinadamu.

117 Unaona, kama nilivyosema katika mahubiri yangu asubuhi ya leo, tunaogopa sana, hata, tunataka Sauli atufundishe,

tunataka Sauli fulani kutoka kwenye seminari atuambie jinsi itupasavyo kuendeleza dini yetu na jinsi itupasavyo kuitekeleza. Hiyo ni ng'ambo ya pili ya Yordani. Ng'ambo hii, Roho Mtakatifu ndiye anayeongoza. Upande huu wewe umetoka kwenye uchafu huo. Upande huu wewe hujali wanalowazia. Upande huu wewe umekufa, na uhai wako umefichwa katika Kristo kwa njia ya . . . na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Hujali. Unaishi katika Kanaani. Unaweza kumudu mahindi magumu. Wewe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Unaelekea kwenye nchi ya ahadi.

118 Ninakumbuka nikisimama kule, Ndugu Collins, kama miaka thelathini iliyopita, wakati kanisa hili halikuwa limejengwa bado. Ulikuwa mkutano mdogo wa hema uliokuwa hapa pembeni, mkutano wangu wa kwanza. Nilikuwa nikihubiri Injili ii hii, jambo lile lile, utajiri wa Kristo usiotafutika, ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, kuamini kila Neno kwamba ni Kweli, ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu, jinsi tu ninavyoihubiri sasa, sijaondoka inchi moja kutoka Kwake. Mungu amenifunulia mengi zaidi juu Yake, kwa hiyo, anaponifunulia, ninazidi tu kulileta. Yeye hatoi kutoka yale yaliyokwisha kuweko, anazidi tu kuongeza mengine mengi juu Yake.

119 Nilisimama kule chini wakati yapata watu mia tano waliposimama ukingoni, wakiimba, "Nasimama kwenye kingo zenye dhoruba za Yordani, na kutupa jicho lenye kutamani, kwenye nchi nzuri na ya furaha ya Kanaani, zilimo mali zangu. Nitafika lini kwenye pwani hiyo ya afya nikabarikiwe milele, nitafika lini nipate kuwa kwenye ninii ya Baba yangu... nikastarehe milele?" Walipoanza kuuimba huo, nilikuwa nikimwingiza mtoni mvulana fulani kumbatiza mle katika Jina la Bwana Yesu. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, ninapomleta mvulana huyu Kwako juu ya kukiri kwake..." Nikiwa mvulana tu, mwenyewe, nina picha hizo nyumbani. Nikasema, "Nikimbatiza kwa maji, Bwana, juu ya kukiri kwake, katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, naomba Wewe ukamjaze na Roho Mtakatifu." Na yapata wakati huo Kitu fulani kikavuma, nayo Hii hapa ikashuka katika upepo wa kisulisuli, ile Nyota ya Asubuhi yenye Kung'aa ikasimama pale. Hapo ikasimama Nuru ile mnayoiona pale kwenye picha. Ikasimama pale.

120 Ilizunguka ulimwengu mzima, huko juu Canada na kila mahali. Wakasema, "Nuru ya ajabu yamtokea mhubiri wa mtaa wa Kibaptisti wakati anabatiza."

121 Siku chache zilizopita, wakati Daktari Lamsa aliponijia, nami sikuwa nimejua chochote kuhusu jambo hilo, naye akaniletea picha, ambayo ndugu anayo pale sasa. Una picha hiyo? Unayo ile Biblia hapo, iko hapo, iko kwenye kitabu chako? Sawa. Kulikuweko na picha ya ishara ya kale ya Kiebrania ya Mungu, ile hasa iliyokuweko katika zamani za Ayubu, kabla Biblia haijaandikwa. Mungu katika sifa Zake tatu, si miungu

watatu. Mungu mmoja katika sifa tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ofisi tatu ambazo Mungu alifanyia kazi. Si miungu watatu, sifa tatu! Nayo Hiyo hapo. Wakati mtu huyo mashuhuri, Daktari Lamsa, tafsiri ya Biblia ya Lamsa, wakati aliposema asubuhi hiyo . . . Nilipomwambia hivyo, nilisema—nilisema, “Ni ishara gani hiyo?”

122 Akasema, “Hiyo ni ishara ya Mungu ya kale, katika Waebrania. Mungu, Mungu mmoja katika sifa tatu.”

Nikasema, “Kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?”

123 Akasimama, kisha akaweka kikombe chake cha kahawa chini, akaniangalia. Gene, naamini ulikuwa pale, Leo. Kasema, “Unaamini jambo hilo?”

Nikasema, “Kwa moyo wangu wote.”

124 Akasema, “Jana usiku, nikisimama katika mkutano wako, Ndugu Branham, niliona huo utambuzi. Sijwahi kuuona hapo awali Marekani, katika nchi yangu.” Akasema, “Hawa Wamarekani hata hawaijui Biblia. Jambo tu wanalojua ni madhehebu yao. Hata hawajui wanakosimama.” Kasema, “Hawajui chochote.” Akasema, “Lakini niliposimama pale jana usiku,” kasema, “nilisema . . . ” Sasa, Ndugu Gene, nasema hili tu kwa uchaji na upendo na kadhalika. Akasema, “Nikasema, ‘Huyo hapana shaka ni nabii.’ Lakini ninapoona kwamba wewe unaamini kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu haikuwa ni miungu watatu, ilikuwa ni sifa, basi najua wewe ni nabii wa Mungu, la sivyo haingalifunuliwa kwako namna hiyo.” Akasema, “Hiyo ni ishara kamilifu.” Kasema, “Mimi kamwe . . . ” Kasema, “Wewe si wa Umoja?”

125 Nikasema, “La, bwana. Mimi si wa Umoja. Namwamini Mungu kuwa ni Mungu Mwenyezi, na zile sifa tatu ni ofisi tatu ambamo huyo Mungu mmoja aliishi.”

126 Akasema, “Nakutakia heri!” Akasema, “Siku moja utamwaga damu yako duniani kwa ajili ya jambo hilo, lakini,” kasema, “manabii daima hufia msimamo wao.”

127 Nami nikasema, “Na iwe hivyo, kama ikimpendeza Bwana wangu.” Tafsiri ya Biblia ya Lamsa.

128 Loo, ni kweli kabisa. Ni mara ngapi, kama ninavyoliambia kanisa hili, kama alivyosema Samueli kabla hawajamchagua Sauli, “Kabla hujaondoka na kujiunga na madhehebu fulani sasa, na kujifunganisha mwenyewe kabisa katika namna fulani ya dini, kwa nini usiache Roho Mtakatifu akuongoze?” Mbona usimchukue Mungu kuwa Kiongozi wako na umwache akubariki, na kusahau dhehebu lako? Sasa, sisemi usiwe mshiriki wa kanisa lolote la kimadhehebu, kuwa mshiriki wa lolote utakalo. Hiyo ni juu yako. Bali ninakwambia wewe, kama mtu binafsi, acha Roho Mtakatifu akuongoze. Soma Biblia. Na lile Biblia isemalo ufanye, lifanye. Mungu awabariki.

129 Na sasa nimengojea muda mrefu sana. Sijui kama kuna yeyote hapa aliyetaka kupitia kwenye mstari wa maombi akaombewe. Iwapo wako, naomba wainue mikono yao. Mmoja tu, wawili, watatu. Vema. Nyote njoni moja kwa moja hapa mkasimame hapa basi mkitaka, wakati huu, na—na tutaomba. Ndipo sisi. . .Bado sitaki mwondoke. Nataka kufanya jambo jingine rasmi hapa kabla tu hatu—hatujafunga.

130 Ni wangapi wanapenda kusoma Kitabu cha Wagalatia. . . loo, namaanisha Waefeso? Sasa, Jumatano usiku, tutaingilia kwenye Muhuri. Kisha asubuhi ya Jumapili ijayo, tutaingilia katika kuliweka kanisa mahali pake. Loo, kama. . .Labda tutaingilia hayo, usiku wa Jumatano hii ijayo, kwenu ninyi watu wa hapa Jeff. Kuliweka kanisa mahali pake walipowekwa, kila mmoja. Jinsi tunavyoitwa kwa kufanywa wana wenye mamlaka. Mungu ametufanya kuwa wanawe wenye mamlaka, sisi ni wanawe kwa kuzaliwa. Tumefanywa wanawe na kuwekwa mahali petu kwa Roho Mtakatifu. Tazama! Kila mmoja wao alikuwa Mwebrania, walipouvuka ule mto, lakini Yoshua aliigawanya ile nchi na kumpa kila mmoja shamba lake kulingana na matamshi ya mamaye alipokuwa anazaliwa, mahali Roho Mtakatifu alipomwambia huyo mama.

131 Hebu mwangalie Yakobo alipokuwa anakufa, nabii, amepofuka, aliikokota miguu yake kitandani, kasema, "Njoni enyi wana wa Yakobo nami nitawaambia mtakapokuwa katika siku ya mwisho." Utukufu! Loo, najua huenda nikaonekana wa ajabu. Watu hawa huenda wakaonekana wa kigeni. Lakini, loo, laiti ungalijua tu ha—hakikisho, kule—kule kuwaka moyo! "Njoni hapa nami nitawaambia mtakapokuwa katika siku za mwisho." Nami naweza kuchukua Andiko lilo hilo, na kuchukua ramani ya mahali Wayahudi wanapokaa leo na kuwathibitishieni ya kwamba wako mahali pale pale ambapo Yakobo alisema watakuwa katika siku ya mwisho. Nao hawajawahi kamwe, hawajawa mahali hapo hata waliporudi kuanzia tarehe saba Mei, 1946, usiku ule yule Malaika wa Bwana aliponitokea kule na akanieleza juu ya huduma hii. Nami naweza kuwaonyesha ya kwamba, waliporejea kwenye nchi hiyo mpya, wao walishika mahali pale pale Yakobo alisema watakaa. Nao ndio hao papo hapo leo. Loo, loo, jamani, loo, jamani! Tumekaribia Nyumbani kwa siku moja zaidi, hiyo tu.

132 Enyi watu wapendwa, ninyi ni wagonjwa, la sivyo hamngekuwa mmesimama hapo kwa ajili ya kusimama tu. Mimi ni ndugu yenu. Nina agizo toka kwa Mungu kuwaombea wagonjwa. Si kama ninii yangu. . .kana kwamba nina nguvu za kuponya, sina. Bali nina nguvu za maombi. Kama nilivyosema asubuhi ya leo, Daudi hakuwa na kitu ila kombeo dogo, bali alisema, "Najua litakalofanya likiwa na nguvu za Mungu juu yake." Unaona? Nina maombi mafupi tu ya kuwaombea, na mikono yangu niweke juu yenu, lakini ninajua yale imani katika

Mungu itafanya. Imewafanyia wengine, itawafanyia ninyi. Basi ninyi aminini hilo sasa mnapojitokeza kuja kupakaribia mahali hapa.

133 Sasa, sijui, kulifanya hili liende vizuri sana, kama nisingemwomba ndugu yangu kuja hapa na kuwatia mafuta. Utafanya hivyo, Ndugu Neville? Nitaliomba kanisa kama mtainama kwa maombi.

134 Sasa kumbukeni, juma lililopita nilipokuwa mgonjwa sana kwa mafuta ya kale ya mbarika, ningalitoa chochote kama mtu angalipita pale na kuniwekea mikono. Kama ningalimpata mtu aje, ambaye Mungu alikuwa amembariki na kumsaidia, ningalifurahia jambo hilo sana. Nyote mnajisikia sasa kama nilivyojisikia mimi wakati huo. Mnajisikia sasa mnataka mimi nifanye jinsi nilivyotaka mtu anifanyie wakati huo. Mungu anizuie nisije nikaepa hiyo kazi. Hebu mimi daima, hata niwe nimechoka, ninapokuwa mchovu, niwapo siwezi kusogeza mguu mmoja kuuondoa kutoka kwa mwingine, acha niende, kwa sababu nitakutana na kila mmoja wenu tena, huko ng'ambo katika Nchi ile kule.

135 Kisha ninyi wanawake wakongwe, wanaume wazee, mliodhoofika, nywele zenye mvi na zinazong'oka, na kupukutika kama waridi ambalo limechanua chipukizi lake dogo, majani yake yanapukutika na yanaanguka ovyo, mnavunjika vipande-vipande, sivyo? Hiyo ni kweli. Ninii tu. . . Na sababu pekee ya kutaka kuishi pamoja ni kunawiri kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kwa hiyo wakati adui amekunyakua sasa na kutoroka, ninakuja na kombeo la Mungu, na imani, na kipawa alichonipa Mungu. Hiki hapa nilichosema, mpate kuelewa. Nilisema, "Kama Petro angaliingia, ama baadhi yao." Usiseme hivyo. Si lazima uniombee. Ingia tu namna hii, na useme, kama kwa mwanamke huyu, useme, "Wewe ni Dada *fulani*?" Jina lako ni nani? Dada Howard. Kasema, "Wewe ni Dada Howard. Wewe ni mwaminio, Dada Howard? Unaamini. Wewe ni mwaminio. Basi, unaona, wewe una haki ya baraka zote za ukombozi." Ndipo ningesema, "Dada Howard, kila kitu kitakuwa shwari," kisha niondoke. Loo, vipi. . . Nikasema, "Ningepiga kelele, ningepaza sauti." Ningesema, "Bwana, haina budi kuwa. Haina budi kuwa."

136 Nami nikawazia, "Vema, watu wanawazia jambo lilo hilo ninapokuja kuwaombea." Kwa hiyo ndivyo ilivyo. Mnaona ninayomaanisha?

137 Nami nimesimama, mara nyingi, na kuwachukua watu, na kusema, "Loo, dada mpendwa, utaliamini? Loo, utaliamini?" "Bwana, Ee Mungu, wafanye waliamini Hilo. Wafanye waliamini." "Loo, tafadhali, utalikubali sasa?" Hilo silo. Nilipita hayo. Nilipita mbali na hayo.

Ninasema tu hivi, "Dada Howard, wewe ni mwaminio?"

"Ndiyo, ni mwaminio."

138 "Vema, Dada Howard, iwapo wewe ni mwaminio, wewe ni mrithi kwa kila kitu alicho nacho Mungu." Na kuchukua tu mkono wake. Mnaona, naamini hilo. Ninawasiliana na Dada Howard kwa kumwekea mikono yangu. Yesu kamwe hakusema "waombeeni," Yeye alisema, "Wawekeeni tu mikono." Ndivyo ilivyo, ndipo anaponywa. Anaweza kusema, "Kila kitu kitakuwa sawa," Dada Howard. Ndipo waweza kwenda nyumbani ukapate afya. Mungu akubariki.

139 Wewe ni Dada . . . [Huyo dada anasema, "Hampton."—Mh.] Dada Hampton, wewe ni mwaminio, sivyo? ["Ndiyo."] Wewe ni mrithi wa kila kitu alicho nacho Yeye. Mungu awe pamoja nawe, Dada Hampton. Nenda nyumbani ukapate afya sasa. Yesu Kristo atakuponya.

140 Wewe ni Dada . . . [Ndugu mmoja anasema, "Slaughter."—Mh.] Slaughter. Hiyo ni . . . Wewe ndiye tuliyekuombea hospitalini. Wewe ni mwaminio, basi, Dada Slaughter, mrithi wa yote tunayoomba. Dada Slaughter, naomba upate ulichoomba, na uwe mzima. Mungu atakujalia.

141 Ndugu Gene, unaamini ya kwamba Mungu atakupa? [Ndugu Gene anasema, "Ndiyo, bwana. Ndiyo, bwana."—Mh.] Na Bwana Mungu akupe, Gene, kile hasa unachoomba! . . . ? . . .

142 Nakujua. [Dada huyo anaongea—Mh.] Wewe ni mwaminio, dada. Nakujua. Huyu ni mume wako hapo. Ndiye niliyemwombea kwa simu siku ile. Siku zote nakumbuka hilo. Hangeweza kwenda kwenye mkutano huko Tulsa. Akaja mkutanoni. Naye Bwana akamponya, akamtuma kwenye mkutano. Katika wakilisho unasimama kwa niaba ya mtu mwingine. ["Mpwa wangu."] Ni jambo la Kikristo jinsi gani, dada! Unaona? Alikuwa mwakilishi pia, alisimama kwa ajili yetu sote. Wewe ni mwaminio na una haki kwa kila kitu ambacho Mungu aliahidi. Mimi ni mtumishi Wake. Na kwa Jina la Yesu Kristo, ninakupa kile unachoomba.

143 Njoo, Ndugu Neil. Mungu akubariki. Imekuwa nzuri sana kwako. Wewe ni mwaminio. Najua ndivyo ulivyo. Ninaamini kwamba Mungu atakupa kila utakaloomba, kwa kuwa wewe ni mwaminio. Na kama mtumishi Wake, kwako, ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, ninakupa haja ya moyo wako. Nenda ukaipokee. Mungu akubariki.

144 Dada Bruce, ninakujua. Yule nesi mdogo aliyenisugua mgongoni alikujua. Anatoka kule chini karibu na Motel JJ, Twin J, ama kitu kama hicho. Utasimama kwa niaba ya wengine. Na unataka nini usiku wa leo kutoka kwa Baba yako? [Dada Bruce anasema, "Kwa ajili yangu mwenyewe, usiku wa leo."—Mh.] Kwa ajili yako mwenyewe, usiku wa leo. [Dada Bruce anazungumza tena.] Basi, adui amekusukuma kupita uwezo wa daktari, lakini ninakufuata, kwa kombeo. Na katika Jina la Yesu

Kristo, ninaelekeza mshale wa kombeo kwenye mwamba ambao umeingia kwenye figo katika hali iliyozuiliwa. Itakurudisha kwa Mungu, kwenye nyumba Yake.

Tumekuomba Wewe, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

145 Wewe ndiwe babake mtu huyu, bwana? Je, wewe ni mwaminio? [Ndugu huyo anazungumza—Mh.] Ngiri ubavuni mwako; chini, na upande wako wa kushoto. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakupa wewe, bwana, na kama mtumishi Wake?

146 Bwana, mkono huu labda umefanya kazi nyingi ngumu za siku. Umekuja hapa kwa kusudi, jambo la kufanya. Mpe, haja ya moyo wake, Baba, ninapoomba katika Jina la Yesu ya kwamba utafanya. Amina.

147 Usiwe na shaka. Hiyo ngiri itakuzuia kuumia huko chini, na utakuwa sawa. Mungu akubariki . . .?. . .

148 [Dada mmoja anasema, "Huumiza kichwa na koo langu, huumiza mbavu zangu ninapokohoa. Siwezi kuimba. Siwezi kufanya chochote. Mimi . . .?. . . Na siwezi kulala sana. Siwezi hata kufanya chochote."—Mh.] Wewe ni mwaminio, sivyo? ["Ndiyo. Nimejazwa na Roho Mtakatifu."] Wewe ni mwaminio. ["Najua kwamba Mungu anakaa ndani."] Na wewe ni—wewe ni mrithi wa baraka hizi zote. ["Najua. Na ninaamini. Ninaamini katika maombi yako, Ndugu Branham. Ninaamini kwamba Mungu ataniponya. Ninaamini kwamba Yeye hujibu maombi yako."] Asante.

149 Baba, ninamleta huyu, dada yangu, kwenye mstari wa moto, katikati ya lengo. Nami ninamrudisha kwako, kutoka kwa mkono wa adui, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

150 Hivyo ndivyo tu itakavyokuwa.

151 [Dada mmoja anasema, " . . .?. . . nina pafu lililokuwa linasimama, na moja lilikuwa limesimama."—Mh.] Upasuaji wa pafu.

152 Ee Bwana, mwanamke huyu kijana anaposimama hapa, angali katika upevu wa ujana, ninamwombea. Na pafu ambalo lingepaswa kutolewa nje, naye angeinama, maisha yake yote. Wewe ni Baba yetu, nami ninalenga moto wa maombi kwake, Bwana, moja kwa moja kwenye pafu hilo. Ninatuma maombi haya katika Jina la Yesu Kristo. Jalia yapige hilo pafu na kuliponya. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba haya. Amina.

153 Wewe ni Dada . . . [Dada huyo anasema, "Dada Gibbs."—Mh.] Dada Gibbs. ["Moja kwa moja kwenye kichwa, na kuwa na maumivu juu yake."] Hasa. Kichwa chako kimevutwa mbali nami. Wewe ni mwaminio na mrithi wa baraka zote za Mungu, Dada Gibbs.

154 Bwana, ninamleta Kwako, na kombeo hili dogo ulilonipa, kama ulivyompa Daudi kombeo, kuwachunga kondoo wa baba

yake. Na kama adui angeingia kufuata kondoo, yeye hakuogopa. Alinyakua kombeo hilo dogo na kuwafuata simba na—na dubu, akawarudisha kondoo. Haya ni maombi ya imani. Uliniambia ikiwa "ningewafanya watu waamini na kuwa waaminifu." Ninamrudisha Dada Gert usiku wa leo. Ninamnyakua kutoka kwa mikono ya adui. Yeye ni kondoo Wako. Ninamrudisha kwenye zizi la Baba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

155 [Dada mmoja anasema, "Dada Lowe."—Mh.] Dada Lowe. ["Nina shinikizo la damu."] Shinikizo kuu la damu. Na wewe ni mwaminio, sivyo, Dada Lowe? Mrithi wa baraka zote.

156 Basi, Baba Mungu, ninalenga maombi haya usiku wa leo, kama kutoka kwenye kombeo la Mungu, kwa ajili ya shinikizo kuu la damu la Dada Lowe. Na naomba wakati mwingine daktari atakapopima shinikizo la damu, na amtazame na kusema, "Ni kawaida sasa." Atajua kilichofanya hivyo. Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa. Amina.

157 [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam. Laiti ningalikuwa na baba yangu hapa usiku wa leo, ningeweza kumwombea sasa hivi. Nitamwombea baba yako, pia. Naelewa.

158 Baba wa Mbinguni, mtu aliyemzaa mvulana huyu, hata yuko hapa duniani usiku wa leo kwa sababu yake. Na mtoto wake mwenyewe anataka baba yake arudishwe; huko nje katika ulimwengu wa dhambi, mlevi. Ee Bwana, ninatuma maombi haya kwa imani na nguvu, na kwa yote niwezayo kulirusha, jiwe hili dogo, katika Jina la Bwana Yesu. Ninamtupia huyo ibilisi ambaye ameweka kitu hicho kushikwa kule. Na iondoke. Na aje salama zizini, katika Jina la Yesu. Amina.

159 [Ndugu mmoja anasema, "Niombee, Ndugu Branham, nipate Roho Mtakatifu. Ninataka kumpokea Roho Mtakatifu. Sina budi kumpokea. Nina shauku. Yanibidi kumpokea Roho Mtakatifu."] Una shauku ya kumpokea. Unataka kuja katika Nchi ziliko ahadi zote. ["Ndiyo."]

160 Na sasa, Bwana, mvulana huyu yuko ng'ambo tu ya mto, amepiga kambi ng'ambo ya pili, na Yordani inavimba. Na hakuna njia kwake kuvuka isipokuwa Wewe utengeneze njia kama vile ulivyomfanyia Yoshua na Israeli. Tena, Baba, ninakuomba, kama mtumishi Wako, mjalie ndugu yetu mpendwa, Ee Mungu, mjalie aingie katika Nchi hii ya ahadi, ahadi hii. Kwamba, upande ule mwingine, kama nilivyobebwa hivi majuzi usiku, naomba nipate fursa ya kumshika na kumkumbatia, katika Nchi hiyo nyingine, nikisema, "Ndugu yangu wa thamani." Tujalie, Bwana. Mjalie apokee ahadi ya Mungu, Roho Mtakatifu. Amina.

161 Ee Bwana, kwake huyu, ndugu yangu mpendwa; mkono huu ambao umekuwa mwema kwangu, na umenifanyia mambo, ambayo hayajasimuliwa. Anaamini na ana imani. Na sasa

adui anajaribu kumnyakua huyu, rafiki yangu: sukari. Naye anafikiri kwamba ana—anaweza kumnyakua mvulana huyu. Lakini ninamfuatilia. Ninakuja, kuwarudisha walio Wako, Bwana, nikirusha jiwe hili kwa imani kamili iliyolenga. Katika Jina la Yesu Kristo ninaupiga ugonjwa huo wa sukari! . . .?. . . ndugu yangu. Warudishe kondoo Wako Mwenyewe kwenye zizi, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada Bell anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]

162 Ee Bwana, dada yetu anajua kuwa uzito huu uliopitiliza ni, kwa hivyo daktari anasema, ndio kitu kinachokuua. "Kila kilo, uzito kupita kiasi, huondoa mwaka mmoja," kulingana na kalenda ya bima. Naye anataka kuishi kwa heshima na sifa ya Mungu. Na hakuna daktari anayeweza kufanya hivi, Baba Mungu. Iko tu m—mkononi Mwako. Naye Dada Bell amekuwa mwaminifu sana. Na amekuwa mkarimu na mwenye kujali katika majaribu, akipitia. Amepitia majaribu mengi mazito. Naja kwa ajili yake usiku wa leo, Bwana. Naja kukutana na adui huyo kule. Ninalenga kwa usahihi wote ambao ninaweza kulenga kwao. Katika Jina la Yesu Kristo ninarusha jiwe hilo la imani kwa adui huyu aliyemshika. Na imtawanye, na kumtorosha mbali naye, naye ataweza kurejeshwa kwenye malisho ya majani mabichi yenye kivuli na maji matulivu, kupitia Yesu Kristo. Amina.

Itakuwa hivyo, Dada Bell. Usiwe tu na shaka.

163 Dada Spencer. [Dada Spencer anasema, "Ndugu, Ndugu Bill, ninampenda Bwana zaidi kila siku ninayoishi. Nami nimekuwa nikija hapa miaka ishirini, mahali hapa. Nami nimeponywa karibu tu kila kitu ambacho kiliwahi kunipata. Unakumbuka yote, na . . .?. . . "—Mh.] Hakika ninakumbuka, dada . . .?. . . ["Naye amenibariki sana! Na ninampenda zaidi, kila siku ya maisha yangu. Najua nina maisha ya ajabu katika Bwana."] Ninaamini jambo hilo, Dada Spencer. ["Nina furaha. Nina furaha! Kama huyu si Roho Mtakatifu niliye naye, ningali—ningali madhabahuni kwa ajili ya kila kitu alichonipa, nami nitafia madhabahuni."] Amina. ["Hilo ndilo ninalotaka afanye na nimekuwa nikifa madhabahuni pamoja na Yesu."] Amina. Mungu akubariki . . .?. . . Amina. ["Nami nitakuambia ninalotaka ufanye. Unajua, Nuhu alichukua familia yake yote pamoja naye, na ninataka familia yangu yote. Unajua nataka wapendwa wangu waokoke."] Naelewa. Watoto wako. Hiyo ni kweli. [" . . .?. . . watoto wangu."] Ndiyo, mama. ["Na mume wangu."] Ndiyo, bwana, mimi . . . ["Kama unavyojua yote juu yake."] Ndiyo. ["Ulituombea."]

164 Sisi sote tunamfahamu Dada Spencer, na kujua ya kwamba jinsi yeye na Ndugu Jess walivyokaa katika hali mbaya, lakini ambapo wameshuka kupitia kanisani hapa. Nikivuka ng'ambo ya pili, hawatakuwa wakitembea hivi. Watakuwa vijana. Loo!

Ndugu Jess, kama mimi tu . . . ? . . . wajua. Na kisha nyote mnajua jinsi, ng'ambo—ng'ambo tu . . . ? . . . kule, unarudi kuwa yule msichana mchanga mpendwa tena, na Ndugu Jess kuwa mvulana mdogo. Mungu alikuahidi.

165 Sasa, tazama. Ninataka kukupa mafundisho kidogo tu, kwa kuwa wewe ndiwe wa mwisho hapa, nataka kutoa.

166 Maana, najua huyu ni mvulana wako mdogo, Charlie. Unataka aombewe? [Ndugu Charlie anasema, "Ndiyo."—Mh.]

167 Nataka kusema jambo hili moja. Je, umewahi kusoma katika Maandiko ambapo Biblia ilisema hili? Paulo alimwambia akida wa Kirumi.

Mnaweza kunisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

168 Alimwambia yule Mrumi, alipouchomoa upanga wake, ajiue, kule Filipi alipokuwa gerezani. Na tetemeko la ardhi likaitikisa jela. Alisema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, na wewe na nyumba yako mtaokolewa." Je, umewahi kusikia hilo? "Wewe na nyumba yako." Sasa, tazama. Ikiwa una imani ya kutosha kwa wokovu kwako mwenyewe, hivi huwezi pia kuwa na imani ya kutosha kwa ajili ya nyumba yako? Mungu, kwa njia fulani, atafanya hilo.

169 Na, Bwana, ninamwombea Dada Spencer na Ndugu Spencer, usiku wa leo, kwamba kila mtoto, wao na watoto wao, wote watakuwa katika hiyo Nchi tukufu, yenye furaha kule ambako hakutakuwa na magonjwa wala uzee, hakuna huzuni wala masikitiko, na maisha haya yote madogo hapa yatafifia na kuwa ndoto mbaya ambayo imepita. Jalia wapokee haya, na jalia watoto wake wote, na mume wake, wapendwa wake wote, na wote wampendao, na wote awapendao, jalia wawe huko pamoja naye, katika Jina la Yesu. Amina.

170 [Dada Spencer anasema, "Amina. Asante."—Mh.] Mungu akubariki. ["Nitakuwa themanini na mbili, hivi karibuni."] Umri wa miaka themanini na miwili. [" . . . ? . . . Lakini wanavunjika, katika umri huo. Lakini bado ninapika, kufua, na kupiga pasi, na kusafisha nyumba."] Kama kwamba tu ulimwengu unasambaratika, Dada Spencer. ["Kweli, ni hivyo. Nimechoka sana, kila wakati. Wanaipata . . . Nilimwuliza mama yangu, mama yangu wa kambo, ambaye alikuwa na umri wa miaka tisini, muda mrefu uliopita. Akasema, 'Rose, labda utakuwa umechoka kila wakati.' Nimechoka."] Vema, uko tayari tu kwenda kupumzika, unaona. ["Nimechoka sana, kila wakati. Nahitaji kupumzika. Nahitaji hilo."] Ndiyo, mama. ["Nami nataka kupumzika katika Bwana, nikiwa nimepiga magoti. Kila, kila kitu ninachohitaji."] Ndiyo. Dumisha tu imani yako moja kwa moja Kwake, Dada Spencer, nawe utavuka. ["Nataka kufia madhabahuni, katika Jina la Yesu. Huyo ndiye ningetaka kumwona, mpaka Yeye aendelee kuita."] Naye akasema . . .

[“Nataka kila kitu alicho nacho Yeye kwa ajili yangu.”] Na kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa pamoja nawe hivi, usiku wa leo, Dada Spencer, kwa neema Yake nitakuona wewe na Jess ng’ambo ya mpaka, vijana na wenye afya tele. Nyote mtakuwa mnakimbia, mkipaza sauti, “Ndugu yangu! Ndugu yangu!” Nitawaona.

Mishipa yake.

171 Baba Mungu, msichana huyu alikuwa na shida, na dawa haiwezi kumsaidia. Kuna yeye tu, kinachozuia. Lakini ninakuja kwa ajili yake usiku wa leo. Naja Kwako, Baba. Naja, nikikuomba uelekeze risasi ambayo inanibidi, itapiga. Na ilengwe kabisa, moja kwa moja mgongoni mwake. Na maombi haya, katika Jina la Yesu Kristo, yapige woga huo na kuupasua vipande-vipande, kuwarudisha kondoo hawa wa malisho ya Mungu. Amina.

Ni lazima tu iwe hivyo, mpenzi.

172 [Dada mmoja anasema, “Omba tu. Nina watoto sita ambao naomba Mungu awaponye na kuwaokoa.”—Mh.]

173 Mungu wa Mbinguni, jalia hilo, watoto wake sita ambao anatamani waokolewe. Amesikia ushuhuda huo wa Ndugu Daulton, binti zake wapendwa. Anatamani watoto wake sita, Baba. Na awe nao. Na wakutane naye katika Nchi ile ambapo hakuna usiku, wamelindwa salama na kuzingirwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Amina.

Naomba uwapate, dada, maombi yangu.

[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]

174 Nakuamini. Hakuna kitu, kabisa, kinachoweza kusaidia. Wanawapa vitu vidogo vinavyoonekana kama, loo, kitu kama asetamini. Ni kotisoni, wanaiita. Hiyo, hiyo inakuua, karibu. Inararua damu yako kabisa. Lakini, tazama. Unaona, ugonjwa wa baridi yabisi ni kama simba aliyekamata kondoo na kukimbia mbali. Sasa, kombeo litafanya nini? Loo, jamani! Kuna simba mkubwa anayenguruma na mwana-kondoo. Naye anampenda mwana-kondoo huyo, kwa hiyo ametoroka na mwana-kondoo. Lakini Daudi akachukua kombeo na kumfuata. Unaona? Sasa tazama. Alikuwa na mawe matano: i-m-a-n-i, yeye mwenyewe, i-n. Kombeo lake lilikuwa katika mkono *huu*: Y-e-s-u. Yeye ni mlenga shabaha hodari. Lazima kitu kitokee. Hebu tufuate ugonjwa huo wa yabisi, usiku wa leo, kwa maombi haya. Mungu akupe.

175 [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Anataka kubatizwa katika Jina? [“Hapana. Hapana. Hakusema hivyo.”] Unataka abatizwe. [“Ni shauku yangu kumwona akibatizwa.”] Asante, dada. Si kwa sababu hiyo ndiyo njia. Ni kwa sababu. . . Sasa, kama hiyo ilikuwa katika Biblia, kwa maana, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” ni—

ningeamini hilo, ningedumu nalo moja kwa moja, dada. Ni—nisingetaka kuwa tofauti hata kidogo. Ni—ningetaka vivyo hivyo. Nisingeruhusu . . . Ni—nitawajibika kwa hilo, unaona. Nami sina budi kusema jinsi tu *Hilo* linavyolisema; sio kuwa tofauti, lakini kuwa mwaminifu.

176 Sasa, Baba, tunakuja kwa ajili ya wapendwa wake ambaye ana ugonjwa wa yabisi, na hapa anataka abatizwe katika Jina la Bwana Yesu, kwa maana huo ndio mlango. Hilo ndilo lango lililofunguliwa. Hapo ndipo Yoshua alipofungua njia moja iliyovuka kuingia katika nchi ya ahadi. Hapakuwa na sehemu mbili au tatu zilizofunguliwa; kulikuwa na moja tu.

177 Petro, Siku ya Pentekoste, wakati Kanisa lilipozinduliwa kwa mara ya kwanza, alifungua njia, kasema, "Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Kamwe hawakutofautiana na njia hiyo hiyo, kila mmoja alivuka hadi kwenye Nchi ya ahadi.

178 Baadhi yao walikuwa wakijaribu kuvuka, chini kabisa kwenye kivuko kingine, ndipo Paulo akamwambia, "Ulibatizwa kwa ubatizo gani? Unajaribu kuvuka wapi?"

Nao wakasema, "Hapa chini ambapo John alitazama."

179 Akasema, "Vema, Yohana alielekeza tu kwa wakati, na mahali." Na ndipo waliposikia hili, wakabatizwa kwenye kivuko sahihi. Nao wakavuka, wakampokea mzabibu wa Roho Mtakatifu.

180 Mjalie dada yetu na wapendwa wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

181 Ndugu Lyle. [Ndugu Lyle anasema, "Ninaamini uko sahihi kabisa chifu, Ndugu Branham."—Mh.] Loo, ndugu! ["Alitembea juu . . . ? . . . Unakumbuka ikiwa kuna katika ndoto, kulikuja kitu . . . ? . . . Ukiitaja ndoto, hiyo ni sawa. Hiyo ndiyo niliyokuwa nayo. Ambapo, umeota kila wakati sawa! . . . ? . . . "] Ndiyo. Hiyo ni kitambo. ["Ndiyo."] Naam. Nina furaha . . . ? . . . Mungu akubariki. Uko njiani kuelekea Nchi ya ahadi sasa! Labda nitataja hilo.

182 Ni wangapi wanakumbuka kabla tu huduma hii haijathibitishwa kwangu, na mimi nikivua samaki na mtu fulani siku moja, chini kwenye mto, ziwa? Nami nilikuwa nikivua samaki wadogo, na Roho Mtakatifu akaja juu yangu. Kulikuwa na . . . Mtu huyu ni Shahidi wa Yehova, alikuwa. Ndugu yake yuko hapa mahali fulani, Banks Wood. Yuko hapa ndani mahali fulani, ambaye ni jirani yangu.

183 Huyu ni Lyle. Na watu hawa walikuwa ni Mashahidi wa Yehova. Nao walisema, siku moja tulipokuwa tukivua samaki kule chini, baada ya mvulana huyu kuongoka, nilimwambia kulikuwa na kitu katika maisha yake, na kile—kile kilichofanyika, na yote kukihusu. Ambapo, ameniambia

sasa hivi tu, na sasa hivi amekiondoa maishani mwake, hiyo ni kweli, chochote kile. Ni kweli kabisa. Baba yake ndiye aliyekuwa m—msomaji. Je, baba yuko hapa usiku wa leo, Billy? [Ndugu mmoja anasema, "Sijui."—Mh.] Na yeye na mke wake, wote wawili, walibatizwa, ili kuwa mashahidi katika Jina la Yesu Kristo, hapa kwenye kidimbwi. Na mtu huyu alikuwa ameketi karibu nami, siku moja.

184 Banks, uko wapi? Je, yuko hapa usiku wa leo? [Ndugu mmoja anasema, "Moja kwa moja nyuma kwenye kona kule nyuma."—Mh.] Nyuma kwenye kona. Ndiyo.

185 Na tulikuwa tukivua samaki. Na, ndugu, mvulana wangu mdogo alikuwa ameua...Nilidhani aliua paka, siku chache kabla. Maskini mama huyo mdogo wa paka alikuwa na kundi la watoto wa paka, naye akamshika na kumwangusha. Niliwazia...Nilisema, "Bwana anaenda kufufua uhai mdogo," siku moja kabla. Hiyo ni kweli, Lyle? [Ndugu Lyle Wood anasema, "Ndiyo."—Mh.] Tukiwa tumeketi kwenye ghuba ndogo. Nami nikasema, "Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI." Na tulivua samaki usiku kucha bila kupata chochote.

186 Asubuhi iliyofuata, tulikuwa tukivua samaki, tumerudi kwenye ghuba ndogo, kwa ajili ya mashavu bluu. Huyo ni samaki mdogo. Naye Ndugu Lyle alikuwa na ufito mkubwa, naye akaacha maskini mashavu bluu kuimeza, ndoano kubwa aliyokuwa nayo, mpaka, alipoitoa, ule uzi mdogo ulikuwa chini kabisa, ndoano kubwa, kwenye maskini tumbo la mashavu bluu. Na wakati alipoitoa, ilimbidi tu kuvuta matumbo na chochote kile kutoka kwenye maskini mashavu bluu, ili kuipata. Na kuitoa tu yote, kwa maana ndoano kubwa ilikuwa imeshikwa kwenye tumbo la samaki huyo. Na alipofanya hivyo, akamtupa chini juu ya maji. Naye alitetemeka tu, mara nne ama tano, na ndivyo ilivyokuwa, kwa maana matumbo yake na mashavu yalikuwa yananing'inia kutoka kinywani mwake. Naye akaelea huko kwa muda wa nusu saa, akaelea akarudi kwenye vichaka.

187 Nami nilikuwa nimeketi pale, nikivua samaki. Ndipo ghafla, Roho Mtakatifu akaja, akasema, "Nena na huyo samaki."

188 Nikasema, "Samaki mdogo, Yesu Kristo anakupa uhai wako tena." Na huyo samaki mdogo, akiwa amelala amekufa juu ya maji, akageuka kwa ubavu wake, kisha akaenda churuuu, kuingia majini, upesi alivyoweza kwenda.

189 Ndugu Lyle na Ndugu Wood walikuwa hapo wameketi. Ndugu Lyle akasema, "Ndugu Branham, hilo lilikuwa kwa ajili yangu, kwa sababu nilimwambia maskini . . . "

190 Usiku wa leo, naweza kuwaambia ulichosema? [Ndugu Lyle Wood anasema, "Hakika unaweza. Ni sawa, Ndugu Branham."—Mh.]

191 Alisema, alipotoa matumbo yake, alimtupa pale, akasema, "Umepumua ya mwisho, ewe jamaa mdogo," hivyo tu. Akamtupa nje.

Akasema, "I—ilimaanisha mimi."

Nami nikasema, "Hapana, Ndugu Lyle. Hiyo haikuwa hivyo."

192 Ndugu Banks kule nyuma, alisema, "Ni watu wangapi katika ulimwengu huu, ni maelfu mangapi, wangependa kusimama mahali tunaposimama sasa hivi, kuona nguvu za Mungu zikishuka na kufanya jambo kama hilo!" Kwa maneno mengine, yeye kama . . .

193 Ninaamini sote tulijisikia kama Petro alivyojisikia, "Ni vizuri kuwa hapa. Hebu tujenge vibanda vitatu." Unaona? Hiyo ni kweli.

194 Sasa, Ndugu Lyle, umetiwa mafuta na Roho Mtakatifu sasa. Umetoka Misri. Vyungu vya vitunguu saumu na uchafu wa dunia umeachwa nyuma. Unasimama chini kwenye ukingo wa Yordani sasa, ng'ambo tu. Mungu na akuvushe; Lyle.

195 Mwenyezi Mungu, hii hapa nyara Yako. Hakika alikuwa katika hali mbaya sana, Bwana, lakini moyo wangu ulimwendea. Maombi yetu yamepiga tu pigo la kuogopesha sana kule, na kitu kile kile kilichomshikilia kimemwondokea. Kimevunjwa. Na sasa anatembea kwenda Yordani. Mpeleke kwenye Nchi ya ahadi, Bwana. Na kumtia muhuri miongoni mwa watu. Kwamba, katika Siku hiyo tukufu tutakapokutana huko, jalia nihisi kukumbatiwa kwa mikono yake, nikipaza sauti, "Ndugu yangu wa thamani!" "Ninamjua Yeye." Mlete Banks pamoja naye, Bwana, sivyo? Baba na mama, na hao wote, dada, na familia hiyo yote kuu, jalia tukutane sote kule, Bwana, na kila mmoja wao ajazwe na Roho Mtakatifu. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Utampokea, ndugu. Mungu akubariki, Ndugu Lyle.

196 [Mtu mmoja anasema, "Ndugu?"—Mh.] Naam, ndugu. ["Kuna simu ya kutoka mbali, na kifo, inayongojea kwenye mstari."]

197 Kuna mtu anakufa, kwenye simu ya kutoka mbali. Nami nitairudisha ibada kwa Ndugu Neville akiwa hapo ndani.

198 [Ndugu Neville anasema, "Siku kuu na ya ajabu katika Bwana! Mungu ametufanyia mambo ya ajabu leo. Matarajio yangu yametimizwa kikamilifu.]

["Tusimame pamoja, kwa miguu yetu.]

199 ["Kumbuka ibada basi, Jumatano usiku. Omba sana. Mioyo yote isiyoridhika, isiyo na uhakika iwe katika mawasiliano sana na Mungu. 'Wakati umekaribia. Sasa ni wakati. Leo ndiyo siku ya wokovu.']

200 [“Mungu awabariki kila mmoja wenu wageni, ninyi watu wa mbali. Maombi yetu ni kwamba Mungu awapeni rehema za safari, kurudi kwenye makazi yenu. Nimefurahia nyinyi kuwa pamoja nasi. Na mtuombee mnapoondoka, ili Bwana abariki mahali hapa pia.]

201 [“Baba yetu wa Mbinguni, kama mtumishi Wako alivyokuja usiku wa leo, kufanya kazi ya ofisi ya mtumishi Wako na nabii, ukisimama katikati, lile pengo, ukitengeneza ua, ukija kwetu kwa shauku inayowaka ya mtumishi Wako, kama tuliobatizwa kwa Roho Mtakatifu, na kupewa ofisi ya unabii, kunena na kizazi hiki. Tusaidie leo na usiku wa leo, kupokea Ujumbe unaotujia, Bwana, himizo, kutayarishwa.]

202 [“Mbariki kila mmoja anayetoka kwenye milango ya jengo hili usiku wa leo. Jalia ugonjwa ulio juu yetu, ambao hatujui lolote kuuhusu, neema na uweza Wako uliobarikiwa na utuhifadhi na kutulinda na kutuponya, na kutudumisha, hadi wakati huo ambapo uko tayari kutuhamisha hadi upande mwingine. Wabariki wote waliokata tamaa na kuvunjika mioyo, waoga na walio dhaifu.]

203 [“Mungu, tunaomba usiku wa leo kwa ajili ya kutembelewa maalum, baraka za Roho Mtakatifu, zikae juu ya kila msafiri, kila msafiri, kila mgeni katika malango yetu. Kila mtu anayetoka mlangoni usiku wa leo, jalia lile pazia la Damu, kutoka msalaba wa Kalvari, lifunike vya kutosha na kutoa.]

204 [“Tuponye tunapokuwa wagonjwa. Utulinde kwa uweza Wako mkuu. Tupake mafuta kwa ajili ya utumishi. Jalia tuenende katika upendo, mbele Zako, siku zote za maisha yetu. Nasi tutakusifu Wewe kwa ajili ya hili, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu Kristo na kwa ajili Yake. Amina.]

205 [“Na Mungu awabariki. Nasi tumefurahi kuwa nanyi. Peaneni mikono nyinyi kwa nyinyi.”—Mh.]

206 Nashukuru sana kwa yote mliyonifanyia, kadi na . . .?. . . Ndiyo, bwana. Kweli nashukuru . . .?. . .

207 Basi tukapeleka jiwe la imani . . .?. . . Kulikuwa na mtu kutoka pande zote . . .?. . . Kwa hiyo nilituma maombi kumfuata, katika Jina la Yesu Kristo. Alikuwa amelala hapo kwa saa moja, hakuna mapigo ya moyo, hakuna pumzi, hakuna chochote. Hakuna pumzi, hakuna mapigo ya moyo, au kupumua, hakuna chochote; macho yakiwa yametua kichwani mwake, alianguka mimbarani. [Ndugu Neville anasema, “Alimwacha tu amelala pale mpaka maombi hayo yakaingia.”—Mh.]

208 *Hii* bado iko wazi? [Ndugu Neville anasema, “Ndiyo, bado inaendelea.”—Mh.]

209 Je, ninaweza kupata usikivu wenu? Huko juu kabisa, mwinjilisti kijana, mhubiri, hapa Indiana, alikuwa akihubiri, alianguka akafa mimbarani, kama saa moja tu iliyopita.

Alipokuwa akihubiri, akaanguka mbele, na akafa mimbarani, mwinjilisti mashuhuri, akihubiri hapa Indiana. Mchungaji amekuja tu na ameniita. Alikufa moja kwa moja wakati akihubiri chini ya upako wa Roho, akaanguka mbele, macho yake yalitulia, pumzi yake ikamwacha. Alitangazwa kuwa amekufa, alikuwa amelala mauti kwa saa moja. Ndipo kitu fulani kikawaambia wapige simu kanisani na kuniomba niombe. Kwa hiyo nilituma maombi kumrudisha, katika Jina la Bwana Yesu. Naomba mjiunge nami kwa imani, kwamba haitakosa shabaha, umfanye upya na kumrudisha. Asante.

210 Mungu awe nanyi, mpaka nitakapowaona Jumatano usiku. Ninyi watu kutoka Georgia na karibu, kwaherini. Mungu awe nanyi.

211 Ndugu Pat...?...

Kufanywa Wana Wenye Mamlaka 1 SWA60-0515E

(Adoption [1])

Mfululizo Wa Kufanywa Wana Wenye Mamlaka

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 15 Mei, 1960, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org